IBADA YA KILA SIKU
NENO LAKO LA KINABII LA KILA SIKU

TOLEO LA 4

Okt – Nov – Des
2025

# HabariNjema
KILA SIKU

**BURE**
HALIUZWI
CHAPISHO HILI LIMELIPIWA NA WASHIRIKA WETU ILI LISAMBAZWE BURE

AMA VILE MAJI YA BARIDI KWA MTU MWENYE KIU, NDIVYO ILIVYO HABARINJEMA ITOKAYO NCHI YA MBALI. (MITHALI 25:25).

Uebert & BeBe
ANGEL

## UEBERT AND BEBE ANGEL



Wakiwa na utajiri mwingi wa uzoefu katika huduma ya wakati wote, Uebert na BeBe Angel wameibuka kama sauti mashuhuri katika kushiriki Habari Njema ya neema ya Mungu ( Euangelion ) na kuendeleza huduma ya kinabii duniani kote. Kama waandishi wanaouzwa sana wa kazi zenye ushawishi kama vile Vita vya Kiroho, Benki za Maombi, Nguvu za Kiungu za Muumini, Grace Driven Life, na Ibada ya HabariNjema Kila siku, wametoa michango mashuhuri kwa fasihi ya Kikristo.

Uebert na BeBe Angel wanaojulikana kwa maono yao, uvumbuzi, na uongozi mahiri ni wazungumzaji wanaotafutwa sana wa mikutano. Kama vinara wa kimataifa na waanzilishi wa The GoodNews Church (Spirit Embassy) na washikilia ofisi ya Nabii, wameathiri kwa kiasi kikubwa mamilioni ya maisha duniani kote, wakisukumwa na kujitolea kwao bila kuyumbayumba katika kueneza ufunuo wa Habari Njema na nguvu ya mabadiliko ya neema ya Mungu (Euangelion ).

## GOODNEWS DAILY DEVOTIONAL

Ibada ya HabariNjema Kila siku ni nyenzo ya Kikristo inayozingatiwa sana ambayo imeandikwa kwa uangalifu ili kutoa utajiri wa kiroho kila siku ya mwaka. Inatoa umaizi wa kina, ufunuo wenye nguvu, na matamko ya kinabii ya kila siku yenye lengo la kuwaongoza wasomaji kuelekea maisha ya Kristo , yaliyokita mizizi katika mafundisho ya mabadiliko na ufunuo wa Nabii Uebert Angel. Yakiwa yanachapishwa kila robo mwaka, ibada hii inatofautishwa kwa namna ya ufikiaji wake wa kimataifa, ambayo inapatikana bila malipo katika lugha nyingi ili kuondokana na vizuizi vya lugha na kuhakikisha kuwa jumbe zake zinazobadilisha maisha zinapatikana kwa wote ulimwenguni.



Jumatano, Oktoba 1

# AKIBA ZA KIROHO

**Marko 1:35**
**Hata alfajiri na mapema sana akaondoka, akatoka akaenda zake mahali pasipokuwa na watu, akaomba huko.**

Mfumo wa benki uko wazi, huwezi kutoa kile ambacho hujawahi kuweka. Mara tu akaunti inapofunguliwa, akiba za kawaida lazima ziwekwe kabla ya kutoa hakujawezekana. Kwa kweli, mtu asiye na akaunti hawezi kutoa chochote.

Kanuni hiyo hiyo inatumika kwenye maombi. Tunaweka akiba za kiroho tunapoomba. Yesu alitumia saa nyingi katika maombi ya alfajiri na mapema, na hadharani, aliamuru tu pepo na magonjwa kuondoka. Benki yake ya maombi ilipakiwa kulingana na Maandiko, mahali Pake pa siri palikuwa eneo lake la kuweka akiba, na huduma Yake ya hadharani ndipo alipokuwa akitoa kwenye akaunti yake, na kusababisha madhihirisho yanayoonekana.

Tumia muda wako kuomba kabla ya kuanza siku yako, na unapoingia ulimwenguni, utakuwa unatoa kwenye akaunti yako, huku ushuhuda ukifuata katika Jina la Yesu.

**TAMKO LA KINABII**
Benki yangu ya kiroho imejaa kikamilifu. Ulimwengu unaonizunguka utaitikia kupitia nguvu ya maombi yangu katika Jina la Yesu Kristo, Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Wathesalonike 5:17

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Obadia 1:10-21; Yona; Mika 1-3



Alhamisi, Oktoba 2

# ONDOA VIKENGEUSHI

**Yohana 18:37**
**... Mimi nimezaliwa kwa ajili ya haya, na kwa ajili ya haya mimi nalikuja ulimwenguni, ili nishuhudie kweli. Kila aliye wa hiyo kweli hunisikia sauti yangu.**

Fokasi ni nguvu inayoyaendesha mafanikio. Pale harakati yako haina vikengeushi, hakika utafikia malengo yako. Lazima ujue kwa nini uko mahali ulipo. Hukuzaliwa ili kuleta msawazo wa mfumo wa ikolojia bali kuathiri Ufalme, familia yako, mahali pa kazi na kwingineko. Adui huwatikisa tu wasio na fokasi, wale wasio na msingi thabiti katika Neno.

Yesu alitangaza kwamba alizaliwa ili aishuhudie ile kweli. Aliishi kwa sababu moja, sio nyingi. Leo, chagua kufokasi kile ambacho ni muhimu sana. Kazini, zingatia kile kinacholeta faida. Lisha mahusiano ambayo ni muhimu zaidi. Kamwe usiruhusu adui aharibu hatima yako kupitia vikengeushi. Viondoe kupitia mafundisho sahihi na fokasi. Kama unaamini Neno hili, kimbia nalo, nawe utarudi na ushuhuda.

**TAMKO LA KINABII**
Nilizaliwa ili kuteka, kushinda, na kufanikiwa katika njia zote. Sitakengeushwa kamwe na adui, kwa maana nimewekwa kwenye njia ambayo ni lazima niifuate katika Jina kuu la Yesu! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Marko 11:23

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Mika 4-7; Nahumu 1-2



Ijumaa, Oktoba 3

# KIONDOA KELELE

**1 Wakorintho 14:10**
**Yamkini ziko sauti za namna nyingi duniani, wala hakuna moja isiyo na maana.**

Vipokea sauti vya masikioni vinavyo ondoa kelele hufanya kazi kwa kugundua mawimbi ya sauti yasiyotakikana na kutoa wimbi la sauti lililogeuzwa (kinyume) ili kuzifuta. Vivyo hivyo, ulimwengu umejaa sauti nyingi, na kulingana na Biblia, hakuna isiyo na maana. Zingine hunyonya nguvu zako na kukuchepusha mbali na njia. Sauti hizi mbaya zinaweza kuja kupitia muziki, mahubiri ya kukatisha tamaa, au mazungumzo yenye uharibifu.

Neno la Mungu ni teknolojia yetu ya kiroho ya kuondoa kelele. Wakati ulimwengu unaposema, “Kuna kuanguka,” unatangaza, “Kuna kuinuliwa.” Jibu kila sauti kinyume na ukweli wa Mungu ili kuondoa kelele. Kunaweza kuwa na mazungumzo ya kushuka kwa uchumi, lakini wewe na familia yako, kataa kushiriki. Wewe ni balozi wa Mbinguni, ugavi wako unatoka kwenye ulimwengu mwingine. Haleluya!

**TAMKO LA KINABII**
Ninaondoa kila neno hasi linalonong’ona masikioni mwangu kwamba sitafanikiwa. Nimeimarishwa katika Neno la Mungu, na hakika nitarudi na ushuhuda wangu katika Jina la Yesu! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Ayubu 22:29

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Nahumu 3; Habakuki 1-3; Sef 1:1-13



Jumamosi, Oktoba 4

# HESABU ZA KIUNGU

**2 Tomotheo 2:15**
**Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali Neno la kweli.**

Kuna shughuli nne za msingi za hesabu: kujumlisha, kutoa, kugawanya na kuzidisha. Kati ya hizi, kugawanya pekee ndiko kunahakikishia sehemu sawa. Ndiyo maana Biblia hutumia "kugawanya" inaposema, "kugawanya kwa usahihi Neno la kweli." Ni hesabu hizi ndugu zangu.

Neno la Mungu lazima ligawanywe kwa usahihi katika kila eneo la maisha yako. Unahitaji afya kama vile unahitaji fedha. Kwa hivyo, usizingatie eneo moja na kupuuza zingine, kwa sababu unavihitaji vyote. Jilishe kwa maandiko yanayoshughulikia nyanja zote za maisha. Panga wakati wa kujifunza sehemu mbalimbali za Neno la Mungu na kujenga mlo wa kiroho wenye usawaziko. Ninaamuru na kutangaza kila eneo la maisha yako litastawi kwa Jina la Yesu!

**TAMKO LA KINABII**
Ninatamka uzima katika fedha zangu, afya, elimu, mahusiano, na kila eneo la maisha yangu. Sitapungukiwa na kitu kizuri. Nimebarikiwa kupita kipimo, katika Jina la Yesu. Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
2 Petro 1:3

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Sef. 1:14-3:20; Hag. 1-2; Zek. 1:1-11



Jumapili, Oktoba 5

# MTAZAMO vs MWINUKO

**1 Wakorintho 15:31**
**Naam, ndugu, kwa huku kujisifu kwangu niliko nako juu yenu katika Kristo Yesu Bwana wetu, ninakufa kila siku.**

Mtazamo wako huamua muinuko wako. Urefu unaofikia katika maisha haya huamuliwa na mtazamo wako. Mtazamo hasi ni msingi wa mahusiano yaliyovunjika, uovu na hasira. Mtume alisema mimi nazika mwili wangu kila siku, maana yake ni asili ya mwili kwenda katika mwelekeo mbaya. Mwili unataka kueleweka, kushinda mabishano, na kufuata mihemuko isiyo na maana.

Unaposoma Neno hili la kinabii, chagua kuzika kila mtazamo mbaya. Itaje kwa majina. Kabiliana nayo. Jiambie kwamba ninazika mtazamo huu mbaya, na uuache. Mitazamo hii hasi inakulemea, lakini leo izike mara moja. Ipo siku njema na kesho kwa ajili yako, lakini mtazamo hasi utaharibu kile ambacho Mungu amekuandalia. Ulizaliwa kwa ajili ya mafanikio, pakua kila mizigo hasi sasa, kwa Jina la Yesu.

**TAMKO LA KINABII**
Ninaondoa kila mtazamo hasi ambao unaniibia furaha, amani na mafanikio yangu. Ninasitisha mkataba wa adui juu ya maisha yangu kwa Jina kuu la Yesu! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Wafilipi4:4

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Zekaria 1:12-7:14



Jumatatu, Oktoba 6

# SAUTI ZA KINABII

**1 Petro 4:11**
**Mtu akisema, na aseme kama mausia ya Mungu; kama mtu akihudumu, na ahudumu kwa nguvu anazojaliwa na Mungu; ili Mungu atukuzwe katika mambo yote kwa Yesu Kristo.**

Ulimi wako sio tu kwa ajili ya kuonja chakula, ni chombo cha Ki-Ungu cha kuunda maisha yajayo unayotamani. Mauti na uzima, pamoja na kufaulu na kutofanikiwa, viko katika uwezo wa ulimi. Utumie kwa busara, na utaunda kesho unayotamani.

Katika huduma yetu, Mungu alitupa vazi la kinabii, lakini maandiko yanatangaza kwamba kila Mkristo anapaswa kunena kama nabii, kama Neno la Mungu.

Leo, kubali ukweli huu: huna haja ya kusubiri mtu mwingine. Zungumza kama nabii juu ya maisha yako mwenyewe. Waruhusu wengine watambue mabadiliko katika jinsi unavyozungumza. Hata kama mambo si mazuri, sema vyema. “Ukata” haupo katika msamiati wangu. Tangaza utele, amani, na ushindi. Viseme, nawe utakula matunda ya maneno yako. Haleluya!

**TAMKO LA KINABII**
Ulimi wangu ni kalamu ya mwandishi tayari. Wema na fadhili zitakuwa fungu langu siku zote za maisha yangu. Chochote ninachotamani, kinatolewa kwa Jina la Yesu. Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Zaburi 45:1

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Zekaria 8-13



Jumanne, Oktoba 7

# INUKA KAMA DUDE

**Yohana 10:17**
**Ndiposa, Baba ananipenda, kwa sababu nautoa uhai wangu ili niutwae tena.**

Kama mzazi au kiongozi, kwa kawaida unawapenda watoto wako kwa sababu wao ni wako, lakini hulka fulani, utii, akili, au mpangilio wa kuzaliwa, kwa mfano, zinaweza kuimarisha upendo huo. Hapa, Yesu anatupa sababu tofauti kwa nini Baba anampenda. Ungemtarajia aseme ni kwa sababu anahubiri au anafanya miujiza, lakini badala yake, anasema, “Kwa sababu nautoa uhai wangu ili niutwae tena.”

Mungu anawapenda wale wanaokataa kukaa chini. Katika ulimwengu uliojaa mateso, kukatishwa tamaa, na vitisho, inuka kama dude lenye nguvu na lisilotikisika. Kuwa mfano wa ustahimilivu. Hata ukihisi kulemewa na kushindwa, kukatishwa tamaa, au kupoteza matumaini, jiambie, “Nikizikwa, sibaki chini, nainuka tena!”

Kuanzia leo, hakuna hali itakuzika. Unainuka kwa Jina la Yesu!

**TAMKO LA KINABII**
Ninakataa kuzikwa na hali au asili yangu. Ninainuka kama pembe ya nyati. Maisha yangu yanalindwa sana na kutetewa sana kwa Jina la Yesu. Haleluya!

**MAFUNZO ZAIDI**
Warumi 4:20-21

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Zekaria 14; Malaki 1-4



Jumatano, Oktoba 8

# MTINDO TOFAUTI

**Warumi 12:2**
**Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu...**

Tunaishi katika ulimwengu ambao kuwa tofauti mara nyingi huepukwa. Wengi hutafuta kupatana na watu wengine, kuwa wa maana, na kuwapendeza watu badala ya Mungu. Lakini Mungu anainua kizazi kinachokataa kuishi kwa viwango vya ulimwengu, kizazi kisichotafuta uthibitisho kutoka kwa ulimwengu. Biblia inatukumbusha kwamba sisi si wa ulimwengu huu, kama vile Yesu hakuwa wa ulimwengu huu.

Kwa sababu tu kitu kinakubalika sana haikifanyi kuwa sawa. Mwangalie Danielii, alichagua njia tofauti. Ingawa wengine walikula kwa anasa, yeye alijiweka kando kwa kumheshimu Mungu, akichagua kula tofauti na wengine.

Sisi ni kizazi kile kinachofuata mtindo tofauti. Hatufananishwi na ulimwengu huu. Hata mawazo yetu yanabadilishwa kwa sababu nia ile ile iliyokuwa ndani ya Kristo sasa iko ndani yetu.

**TAMKO LA KINABII**
Mimi si wa ulimwengu huu. Nimetengwa kwa kusudi takatifu la Mungu. Mimi ni nuru angavu na ing'aayo mbele ya watu kwa utukufu wa Baba yangu wa Mbinguni. Amina!

**MAFUNZO ZAIDI**
Yohana 15:19

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Mathayo 1-4



Alhamisi, Oktoba 9

# NANI YUPO PAMOJA NAWE?

**2 Tomotheo 4:11**
**Luka pekee yake yupo hapa pamoja nami. Umtwae Marko, umlete pamoja nawe, maana anifaa kwa utumishi.**

Kuna aina tatu za watu maishani: wale wanaokuja kwa sababu, somo, au msimu. Nimezipitia zote. Wale wanaokuja kwa sababu husaidia kutimiza maono yako. Wale wanaokuja kwa ajili ya msimu fulani wamepewa na Mungu kukuhudumia na kukutegemeza kwa ajili ya majira hayo. Halafu kuna wanaokuja kukupa somo. Laweza kuwa somo chanya au hasi, wakati mwingine hata kupitia maumivu unapaswa kuwa na busara zaidi.

Mtume Paulo alisema Marko alikuwa wa faida kwake. Alikuwa hazina ya manufaa. Alileta urahisi, si maumivu au mzigo. Leo naomba Mungu akutumie wasaidizi wa Ki-Ungu wanaokuja kwa sababu fulani, nawe utembee katika hekima kamili ya kuwatambua na kuwakubali. Amina.

**TAMKO LA KINABII**
Ninaamuru wasaidizi wangu wa Ki-Ungu waje kutoka kila upande. Ninang'oa kila mbegu hasi ya nishati iliyopandwa karibu nami, katika Jina la Yesu! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Wakolosai 3:17

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Mathayo 5-7



Ijumaa, Oktoba 10

# PESA YENYE UTUME

**Zekaria 1:17**
**Bwana wa majeshi asema hivi; Miji yangu kwa kufanikiwa itaenezwa huko na huko; naye Bwana ataufariji Sayuni tena, atauchagua Yerusalemu tena.**

Injili ni bure, lakini njia ya kuifikisha kwa watu sio bure. Kwa neema ya Mungu, tunaendesha huduma ya mabilioni ya dola, kulisha wenye njaa, kupeleka baadhi shuleni, kuchapisha nyenzo za uinjilisti, na kuandaa makusanyiko ya kidini, ambayo yote yanahitaji fedha. Unaweza kuwa unasoma ujumbe huu wa kinabii bila malipo, lakini mtu fulani alilipia ili uchapishwe.

Ufalme wa Mungu unahitaji rasilimali ili kuuendeleza. Ndio maana Mungu anatamani ufanikiwe kiuchumi. Akasema, "Miji yangu kwa kufanikiwa itaenea." Unapojaribu kuunda himaya kubwa ya kifedha, usifanye kwa sababu za ubinafsi, acha iwe pesa ya misheni. Mtu anapaswa kula kwa sababu Mungu alikubariki na fedha. Kanisa mahali fulani linapaswa kujengwa kwa sababu ya mafanikio yako.

Pokea baraka za kifedha leo. Pesa zinakuja!

**TAMKO LA KINABII**
Pesa yangu inakuja! Ninapata rasilimali za kifedha kwa manufaa ya Ufalme. Milango yangu yote iko wazi kupokea mavuno kwa Jina la Yesu! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Mithali 3:9

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Mathayo 8:1-10:15



Jumamosi, Oktoba 11

# MAONO

**1 Mambo ya Nyakati 26:18**
**Penye Parbari upande wa magharibi, walikuwapo wanne darajani, na wawili huko Parbari.**

Maono ndiyo nguvu inayoongoza nyuma ya kila mafanikio. Maandiko yanasema, “Pasipo maono, watu huacha kujizuia.” Hicho si kifo cha kimwili tu, bali kifo cha chochote unachogusa. Maono huelekeza juhudi zako kuelekea lengo lililobainishwa na matokeo yanayotarajiwa.

Chukua andiko lililo hapo juu: wengi hufikiri kwamba walinzi waliwekwa baada ya hekalu kujengwa, lakini nabii aliwaona wakiwa wamesimama kwenye malango muda mrefu kabla ya ujenzi kuanza. Huenda huna nyumba sasa, lakini wazia familia yako katika jumba kubwa, akaunti yako ya benki ikifurika, huduma yako inastawi. Uwezo wako wa mawazopicha ni uwezo wako wa ubunifu.

Wazia jambo unalotamani, lifanyie kazi, na utafurahia matunda ya maono yako.

**TAMKO LA KINABII**
Kikombe changu kinafurika. Ninaishi maisha ya maziwa na asali, hakuna kinachokosekana na hakuna kilichovunjika. Mungu yu pamoja nami, sitapungukiwa na kitu chochote chema. Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Mithali 29:18

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Mathayo 10:16-12:21



Jumapili, Oktoba 12

# UKOMBOZI MKUU

**Hosea 4:6**
**Watu wangu wanaangamizwa kwa kukosa maarifa; kwa kuwa wewe umeyakataa maarifa, mimi nami nitakukataa wewe...**

Watu wengi wanafikiri ukombozi ni pale mtu anapogalagala sakafuni, kulia, au kutapika kanisani. Lakini nisikieni ndugu zangu, kufunguliwa kwa kweli hutokea pale ujinga wenu unapokabiliwa. Unaweza kugalagala kwenye sakafu na bado ukainuka bila kubadilika.
Ibilisi anaitwa mkuu wa giza, "mkuu" akimaanisha wa kwanza, na "giza" maana yake ni ujinga. Alikuwa wa kwanza kuwa mjinga.

Kataa ujinga. Pokea nuru kupitia Neno la Mungu. Neno huleta nuru inayoondoa giza na kubadilisha fikra zako. Wakati mawazo yako yanabadilika, wewe ni huru kweli kweli. Ujuzi kutoka kwenye Neno hukukomboa wewe vizuri kuliko kitu kingine chochote.
Lisha Neno la Mungu, na ujinga utakukimbia. Fedha zako, wito, afya, na kila eneo litastawi wakati nuru inakuja kupitia Neno.

**TAMKO LA KINABII**
Ninakataa kuishi katika ujinga. Kupitia Kristo, mimi ni huru na si mtumwa wa ujinga tena. Nia hiyo hiyo iliyokuwa ndani ya Kristo iko ndani yangu; maarifa na ufahamu hutiririka kutoka ndani yangu katika Jina la Yesu. Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Zaburi 119:130

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Mathayo 12:22-14:12



Jumatatu, Oktoba 13

# VIUMBE WA AJABU

**1 Petro 1:10**
**Katika habari ya wokovu huo manabii walitafutatafuta na kuchunguzachunguza, ambao waliotabiri habari za neema itakayowafikia ninyi.**

Nilipokuwa mdogo, nilijiita “Eliya Mweusi.” Wakati huo, nilifikiri nguvu za Eliya zilikuwa zaidi ya chochote ningeweza kuwazia hadi Mungu alipoanza kunifunulia kweli za ndani zaidi kupitia andiko la leo. Hata manabii kama Eliya walitamani kutazama katika mafumbo ya ajabu ya wokovu, lakini hawakupewa ufikiaji. Ilikuwa ni zaidi ya kueleweka kwa manabii wa kale kuamini kwamba aina mpya ya kiumbe kingekuja, ambacho ndani yake Mungu Mwenyewe angekaa.

Katika Agano la Kale, Roho Mtakatifu aliwajilia manabii kwa muda ili wao watabiri. Lakini sasa, Mungu amefanya makao yake ya kudumu ndani yetu. Anaishi ndani yako na mimi. Hiyo ina maana sisi ni wakuu kuliko Eliya au Isaya. Kwa ufunuo huu, nenda nje na ushinde ulimwengu wako kupitia nguvu za Roho Mtakatifu. Amina.

**TAMKO LA KINABII**
Kristo ndani yangu ndiye tumaini la utukufu wote. Mimi ni nyumba yenye nguvu ya Ki-Ungu, na kila kitu kunihusu kinageuka kwa utukufu wa Mungu katika Jina la Yesu. Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Waebrania 11:39-40

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Mathayo 14:13-17:13



Jumanne, Oktoba 14

# KANISA LA WASHINDI

**Warumi 8:37**
**Lakini katika mambo hayo yote tunashinda, na zaidi ya kushinda, kwa yeye aliyetupenda.**
Kuna aina tatu za makanisa au Wakristo: walioshindwa, wapiganaji na washindi. Kanisa lililoshindwa halijatambua haki zao kamili katika Kristo. Kanisa la wapiganaji daima linapigana na mapepo na kutafuta ukombozi. Lakini Kanisa la ushindi limesonga zaidi ya kiwango cha mapigano, wanafanya kazi kutoka kwenye mtazamo wa kilele cha mlima.

Wakristo washindi wanabadilishwa kabisa na Neno na kujaa ufahamu. Hawatazamii tena ukombozi; badala yake, wanatafuta wengine ili kuwaweka huru. Hawa ni majemadari wa Mungu, wenye nguvu katika maombi na kusherehekea Neno. Kua na kuwa Mkristo mwenye ushindi. Wewe si dhaifu; wewe ni jenerali kwa haki yako mwenyewe.

**TAMKO LA KINABII**
Nina mtazamo wa kilele cha mlima; Ninaishi juu ya hali ya maisha haya. Mimi si yule aliyeshindwa au anayehitaji ukombozi, mimi ni Kanisa lenye ushindi! Ninaamuru kwamba mamlaka yangu katika Kristo ni hai na dhahiri. Ninatembea katika utawala, ninaongoza wengine katika uhuru, na kutekeleza ushindi wa msalaba katika kila eneo la maisha. Ustawi wangu, amani, na uwezo wangu havitikisiki katika Jina la Yesu! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
2 Wakorintho 5:20

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Mathayo 17:14-20:34



Jumatano, Oktoba 15

# EKKLESIA

**Mathayo 16:18**
**Nami nakuambia, Wewe ndiwe Petro, na juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu; wala milango ya kuzimu haitalishinda.**

Kanisa ni nguvu kubwa zaidi duniani. Wengine kwa ujinga huonyesha Kanisa kama mkusanyiko wa waumini waoga wanaomlilia Mungu. Lakini tuko mbali zaidi. Neno "Kanisa" linatokana na neno la Kigiriki Ekklesia, linalomaanisha mkusanyiko wa watu wanaofanya maamuzi ya kiserikali. Kanisa huamua jinsi mambo yanapaswa kuenenda katika mataifa.

Hii ina maana kuna uweza, nguvu, na mamlaka katika jumuiya ya Wakristo. Wewe ni sehemu ya bodi ya sheria yenye nguvu zaidi iliyopo. Kuhudhuria kanisa sio kawaida tu; ni mahali ambapo hatima huimarishwa, na kanuni na sheria zinazotawala ulimwengu zinarekebishwa. Kwa hiyo, usikae pembeni; kuwa miongoni mwa wafanya maamuzi na washawishi katika Kristo. Wafute kazi wale wanaohitaji kufutwa kazi, na kuwaweka wale ambao wanahitaji kuwekwa katika nafasi. Umepewa uwezo wa kupanda na kung'oa chochote unachotaka, kwa Jina kuu la Yesu!

**TAMKO LA KINABII**
Mimi ni sehemu ya Ekklesia ya Mungu, baraza linaloongoza lenye nguvu zaidi Duniani. Ninatunga sheria katika roho na kuweka utaratibu wa Ki-Ungu katika Mataifa. Milango ya kuzimu haitanishinda kwa Jina kuu la Yesu! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Waebrania 10:25

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Mathayo 21-22



Alhamisi, Oktoba 16

# MUHUDUMU WA KUFURAHIA

**Wafilipi4:4**
**Furahini katika Bwana sikuzote; tena nasema, Furahini.**

Jukumu la furaha yako si la mtu mwingine yeyote, ni kazi uliyopewa na Mungu. Mtu mwenye furaha hawezi kukabiliwa na huzuni, magonjwa, na kukata tamaa. Kamwe usilaumu wengine kwa uhasi wowote unaotokea karibu nawe. Adui atakupa sababu za kuendelea kushindwa kwa kukushawishi kuwanyooshea wengine vidole. Kuhamisha lawama ni mbinu ya adui kukufanya uendelee kukwama.

Maandiko ya leo yanakuagiza furahi katika Bwana. Kristo ndani yako ndiye tumaini la utukufu. Haijalishi ni nini kilifanyika katika siku zako zilizopita, futa machozi yako, binua mabega yako, na usonge mbele. Una chemichemi za uzima ndani yako, ziruhusu kutiririka katika kila eneo la maisha yako. Lisha Neno la Mungu, na nuru yake itaangazia kila kona ya giza. Rejesha furaha na nguvu zako sasa, katika Jina la Yesu!

**TAMKO LA KINABII**
Maisha yangu yanalindwa na nguvu kutoka juu. Ninakataa kuwa dhaifu, mwoga, au mwenye hofu. Hakuna hali inayoweza kuiba furaha yangu. Ninachukua jukumu kamili la furaha yangu na kuachilia chemichemi za maisha ndani yangu. Nafurahi katika Bwana siku zote! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Nehemia 8:10

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Mathayo 23:1-25:13



Ijumaa, Oktoba 17

# USIMAMIZI

**Luka 16:11**
**Basi, kama ninyi hamkuwa waaminifu katika mali ya udhalimu, ni nani atakayewapa amana mali ya kweli?**

Kila unachokisimamia vibaya, Mungu atakiondoa kutoka kwako. Ikiwa utatumia pesa vibaya, itaondolewa. Kila tajiri ni uthibitisho wa uwakili wa Ki-Mungu wa rasilimali za kifedha. Biblia hata inasema usipoweza kutumia pesa vizuri, Mungu hatakuamini kwa karama na baraka za rohoni.

Fanya uamuzi wa makusudi wa kusimamia maisha yako ipasavyo. Pangilia na ugawanye muda wako, kutoka kwenye maombi hadi kazi, kwa busara. Usichanganye vipaumbele vyako. Simamia mambo yote vizuri, na Mungu atakusaidia kupata mengi zaidi. Unaposoma ujumbe huu wa kinabii, neema ya kusimamia huduma yako, familia, na fedha inakuja juu yako.

**TAMKO LA KINABII**
Neema ya Bwana i juu yangu, na amenikabidhi baraka za kimwili na za rohoni. Ninafanya kazi kwa hekima na nidhamu ya Ki-Ungu. Ninasimamia kila rasilimali, muda, pesa, huduma, na mahusiano kwa ubora. Mimi ni msimamizi mwaminifu, na makubwa zaidi yanaachiliwa mikononi mwangu, katika Jina la Yesu. Amina!

**MAFUNZO ZAIDI**
Zaburi 90:12

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Mathayo 25:14-26:68



Jumamosi, Oktoba 18

# MUNGU KATIKA KIFICHO

**2 Wakorintho 4:7**
**Lakini tuna hazina hii katika vyombo vya udongo, ili adhama kuu ya uwezo iwe ya Mungu, wala si kutoka kwetu.**

Mojawapo ya makosa makubwa zaidi ni kuamini kuwa wewe si wa maana mbele za Mungu. Mungu anapokutazama anajiona. Mtume Paulo anafunua kwamba tunabeba hazina ndani ya miili yetu ya duniani. Umbo lako la kimwili huweka hazina za Ki-Ungu, Mungu Mwenyewe! Wewe ni Mungu katika kificho!

Kuanzia leo, anza kusema na kuishi kama mtu aliyembeba Mungu. Wewe u mbali na ukawaida, na mafanikio yako yamehakikishwa. Unapozungumza, ongea kwa mamlaka, ukijua wewe ni Neno la Mungu na kuna akiba ya uzima na nguvu ndani yako.

**TAMKO LA KINABII**
Mimi ni Mungu katika kificho, nguvu zake hukaa ndani yangu! Njia na mipango yangu ni mipango ya Mungu. Mimi ni mbeba hazina za Ki-Ungu, na kila ninachogusa leo kimebarikiwa. Ninazungumza kwa mamlaka ya Mbinguni, na ninadhihirisha ubora wa Mungu katika yote ninayofanya, katika Jina kuu la Yesu! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Zaburi 82:6

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Mathayo 26:69-28:20



Jumapili, Oktoba 19

# WAZAO WA MUNGU

**1 Petro 1:23**
**Kwa kuwa mmezaliwa mara ya pili, si kwa mbegu iharibikayo, bali kwa ile isiyoharibika, kwa neno la Mungu lenye uzima, lidumulo hata milele.**

Siku zote huwa nawaambia watu kuwa ukifokasi sana kwenye jana yako, utaishia kuileta jana yako kwenye viunga vyako. Wengi husingizia kushindwa kwao kwa kulaumu jana zao au laana za familia. Lakini unapokuja kwa Yesu Kristo, unakuwa kiumbe kipya, kilichozaliwa kwa mbegu isiyoharibika ambayo ina kinga dhidi ya laana.

Chukua hatamu kamili ya maisha yako na lifanyie kazi Neno. Acha ukweli huu wa sasa ushike mawazo yako: sasa wewe ni wa kusanyiko tukufu la wale walioitwa. Hakuna umaskini, kushindwa, au magonjwa katika maisha yako, kwa jina kuu la Yesu!

**TAMKO LA KINABII**
Nimechaguliwa na Mungu, nimetengwa na kufanywa Mtakatifu kwa kusudi la Ki-Ungu. Nimezaliwa kwa mbegu isiyoharibika, kinga dhidi ya kila laana na mipaka. Ninaishi juu ya mifumo ya ulimwengu huu, hakuna tena umaskini, kushindwa, au magonjwa. Ninatembea katika ushindi, na mafanikio yangu yamehakikishwa, katika Jina la Yesu! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
1 Petro 2:9

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Marko 1-3



Jumatatu, Oktoba 20

# YA HIVI PUNDE ZAIDI

**1 Petro 1:12**
**Wakafunuliwa ya kuwa si kwa ajili yao wenyewe...**

Mungu ametupa upendeleo wa kuwa wadau wakuu wa unabii. Kwa neema yake, tumetoa unabii usiohesabika, wa kimataifa na wa mtu binafsi; yote yametimia. Kila video ya kinabii tunayotoa ina saini hii: “Ya hivi punde zaidi kuliko gazeti la kesho, kwa hisani ya Roho Mtakatifu.” Kwa nini? Kwa sababu usahihi huo unawezekana tu kwa uwezo wa Roho wa Mungu.

Maandiko ya leo yanafichua ikiwa kuna ukweli wa sasa, basi lazima pia kuwe na ukweli uliopita na ujao. La kusikitisha, Wakristo wengi wanaishi katika ukweli wa zamani. Hawajui kwamba uponyaji na baraka zote za kiroho tayari ni zao katika Kristo.

Unapositawisha uhusiano na Roho Mtakatifu, Yeye hukuweka kuwa wa sasa, sahihi, na mwenye taarifa kuhusu fedha zako, huduma, biashara, na maeneo yote. Weka muda katika Neno na maombi kila siku, na wewe, pia, utakuwa wa hivi punde zaidi kuliko gazeti la kesho.

**TAMKO LA KINABII**
Wakati ujao wangu ni salama, kwa kuwa ninatembea katika mapenzi makamilifu ya Mungu. Kushindwa sio sehemu yangu. Siku zote nitajua la kufanya, wakati wa kufanya, na jinsi ya kufanya, katika Jina la Yesu. Amina!

**MAFUNZO ZAIDI**
Zaburi 37:23

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Marko 4-5



Jumanne, Oktoba 21

# TIMU YA WATANGULIZI

**Marko 1:35**
**Hata alfajiri na mapema sana, akatoka akaenda zake mahali pasipokuwa na watu, akaomba huko.**

Kabla ya rais yeyote au mtu mashuhuri kutembelea eneo, timu ya watangulizi hutangulia kuvinjari mahali na kuhakikisha kuwa kila kitu kiko sawa. Timu hii hutambua na kuepusha hatari zinazoweza kutokea. Vivyo hivyo, katika mwendo wetu wa imani, tuna timu yetu ya watangulizi, maombi. Maombi ni timu ya itifaki ya kiroho ambayo huenda mbele yetu kuandaa na kulinda njia yetu na kurekebisha shida yoyote.

Yesu aliamka asubuhi na mapema ili kuomba, akituma itifaki yake mbele ili kukabiliana na changamoto na magonjwa kabla ya kukutana nazo. Maombi yalimweka kwenye nafasi ya ushindi kabla ya siku kuanza. Chukua muda wa kuomba sasa. Tuma majeshi ya kiroho yatangulie kutengeneza siku yako na kupata matokeo yako, katika Jina la Yesu.

**TAMKO LA KINABII**
Ninatuma maombi katika maisha yangu yajayo; njia yangu ni salama, na maisha yangu yako sawa. Kila hatua ninayopiga imepangwa kwa ajili ya ushindi. Ninaweka wasaidizi wa Ki-Ungu katika maeneo ya kimkakati, na hakuna kizuizi kinachoweza kustahimili uwezo wa timu yangu ya watangulizi. Muujiza wangu umehakikishwa, katika Jina la Yesu! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Kutoka 23:23

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Marko 6-7



Jumatano, Oktoba 22

# UKUU WA NENO

**Zaburi 138:2**
**Nitasujudu nikilikabili hekalu lako takatifu, Nitalishukuru jina lako, kwa ajili ya fadhili zako na uaminifu wako, kwa maana umeikuza ahadi yako, kuliko jina lako lote.**

Kuna jambo moja tu ambalo Mungu alitupa ili kumlaghai Yeye na mifumo Yake: ni Neno Lake. Hatumlaghai Mungu kwa uwezo wetu wenyewe, bali kwa sababu aliiweka iwe hivyo. Kwa kadiri Jina Lake lilivyo juu ya kila jina lingine Mbinguni na Duniani, kuna kitu alichoweka juu zaidi, Neno Lake.

Mungu anatenda kazi ndani ya mipaka ya Neno Lake na hafanyi kazi nje ya neno. Zaburi 138:2 inasema Amelikuza Neno Lake kuliko Jina Lake. Kwa hivyo, ukitafuta Neno, unapata uwezo wa kutawala mifumo ya kiroho. Omba kulingana na Neno Lake, na sheria za kiroho humlazimisha Mungu kutoa kile alichosema katika Neno Lake.

Liendee Neno, na hakika utarudi na ushuhuda.

**TAMKO LA KINABII**
Neno la Mungu ni kuu, linatosha, na lina nguvu katika asili yake. Ninachagua kuliendea Neno, na ushuhuda wangu umehakikishwa. Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Waebrania 4:12

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Marko 8:1-10:12



Alhamisi, Oktoba 23

# PARAPANDA YA MWISHO

**1 Wakorintho 15:52**
**kwa dakika moja, kufumba na kufumbua, wakati wa parapanda ya mwisho;**

Biblia inapotaja "parapanda ya mwisho," inadokeza kwamba kulikuwa na zingine kabla yake. Parapanda hii ya mwisho italia kwenye unyakuo, na ninaomba uweko kwenye safari ya kwanza. Lakini ikiwa kuna parapanda ya mwisho, swali langu ni, ni lini tulisikia zile za mwanzo?

Ndugu na dada, kuna parapanda nyingi zinazosikika karibu nasi hata sasa, na wakati mwingine tunasahau kuzizingatia au kuzipuuza. Neno tunalohubiri kuhusu unyakuo unaokaribia tayari ni parapanda. Rafiki yako anapokuhimiza uombe, au mwenzi wako anakuonya ukate uhusiano fulani, hizo ni parapanda pia. Zingatia kila baragumu, na utafaulu hadi unyakuo wakati Bwana atakapokuita nyumbani.

**TAMKO LA KINABII**
Roho yangu i hai na imeamka; Sitaikosa sauti yoyote muhimu karibu nami. Ninasonga juu na sishuki chini kwa Jina la Yesu. Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Amosi 6:1

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Marko 10:13-12:12




Ijumaa, Oktoba 24

# ROHO KAMA YA MTOTO

**Luka 18:16**
**Bali Yesu akawaita waje kwake, akasema, Waacheni watoto wadogo waje kwangu, wala msiwazuie, kwa kuwa watu kama hao Ufalme wa Mungu ni wao.**

Umewahi kuona jinsi mtoto mdogo anaweza kuamini chochote unachomwambia? Ukisema unaenda kufanya manunuzi na utamletea ndege ya kweli, atakungoja kwa matarajio kamili. Shaka haipo katika ulimwengu wa mtoto; kila neno linachukuliwa kuwa kweli.

Ufalme wa Mungu si wa wenye nia mbili bali kwa wale walio na imani kama ya mtoto, wale wanaoamini kikamilifu kile anachosema Mungu na hawawezi kamwe kutikiswa. Mambo ya kiroho hayahitaji mantiki; hayaleti maana, lakini yanafanya imani. Ondoa mashaka na dhana potofu leo, na imani yako italeta matokeo kwa Jina la Yesu.

**TAMKO LA KINABII**
Moyo na roho yangu viko tayari kupokea kila baraka ambazo Mungu amenijalia. Ninaamini kwa imani kama ya mtoto, bila shaka au kusitasita. Ninatembea katika matarajio kamili na nitaishi kwa utele, katika Jina la Yesu! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
1 Yohana 5:14-15

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Marko 12:13-14:11



Jumamosi, Oktoba 25

# AHADI KAMILI YA MUNGU

**Waefeso 1:23**
**Ndilo mwili wake, ukamilifu wake anayekamilika kwa vyote katika vyote.**

Watu wengi bado wanaishi katika ukweli wa Agano la Kale. Wako katika hali ya kuamuru ahadi za Mungu zionekane katika maisha yao. Lakini je, kweli kuna ahadi ambayo Mungu alitupa? Huenda ukawa na mawazo mengi kuhusu yale unayoamini kuwa ni ahadi za Mungu. Ukweli ni kwetu sisi Wakristo wa Agano Jipya, hakuna ahadi isipokuwa Yesu Kristo Mwenyewe.

Katika Kristo tunapokea kila baraka na ahadi tunazoweza kuhitaji. Yeye ndiye utimilifu wa Uungu, kielelezo cha baraka zote za kidunia na za mbinguni. Unapokuwa na Kristo, una kila kitu! Sasa ni jukumu lako kuamsha na kudhihirisha baraka ambayo Mungu alikupa kupitia Kristo ili kudhihirisha.

Kupitia maombi, kujifunza Neno, na kufuata kanuni zake, kila baraka na ahadi katika Kristo itadhihirika katika maisha yako.

**TAMKO LA KINABII**
Kristo ndani yangu ndiye tumaini la utukufu wote. Ndani Yake, kila ahadi inatimizwa, na kila baraka imekamilika. Sitapungukiwa na kitu chochote kizuri katika Jina la Yesu! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Wakolosai 1:27

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Marko 14:12-15:47



Jumapili, Oktoba 26

# UTAJIRI USIOPIMIKA

**Waefeso 3:8**
**Mimi niliye mdogo kuliko yeye aliye mdogo wa watakatifu wote, nimepewa neema hii ya kuwahubiri mataifa utajiri wake Kristo usiopimika;**

Mataifa kote ulimwenguni yanapigania kila siku haki ya madini. Uvumbuzi wa amana mpya unafanywa kila msimu. Hata hivyo, hizi ni sehemu ndogo tu ya baraka za Mungu duniani. Biblia inazungumza juu ya utajiri usiochunguzika wa Kristo, mgao usio na mwisho wa utajiri unaopatikana ndani Yake. Huu ni ustawi wa pande zote, unaojumuisha afya yako, fedha, na zaidi.

Unapompokea Yesu Kristo, si desturi ya kiroho tu bali ni badiliko kamili la maisha ya utele na amani. Ninaamuru na kutangaza juu ya maisha yako kwamba chochote unachotaka ambacho kinaendana na Neno la Mungu kinatolewa kwa Jina la Yesu.

**TAMKO LA KINABII**
Ninakunywa kutoka kwa visima vya wokovu na kila kitu kunihusu kinaangukia mahali pazuri. Ninachota kila kitu ninachohitaji na kutamani kutoka kwenye utajiri usiopimika wa Kristo. Kila ahadi ya Mungu kwangu katika Kristo ni ‘Ndiyo!’ na ‘Amina!’

**MAFUNZO ZAIDI**
2 Petro 1:3

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Marko 16; Luka 1



Jumatatu, Oktoba 27

# MBALI ZAIDI KUPITA BINADAMU

**2 Wakorintho 5:17**
**Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita; tazama! Yamekuwa mapya.**

Viwango vya mwanadamu vipo kwenye hatari ya kila aina ya majanga na kushindwa. Moja ya mikakati muhimu ya adui ni kukukumbusha kuwa wewe ni mwanadamu tu, umezaliwa kwa nyama na damu. Ukishakubali hilo, unajisalimisha kwa mungu wa dunia hii, na kushindwa kunakuwa ni jambo lisiloepukika.

Maandiko, hata hivyo, yanasema wewe ni kiumbe kipya ndani ya Kristo, mbali zaidi kupita mwanadamu. Neno la Kigiriki ni kainós , ambalo linamaanisha kitu kipya kabisa ambacho hakijawahi kuwepo hapo awali. Huenda ulitenda dhambi jana tu au hata saa chache zilizopita, lakini acha ukweli huu ukite mizizi: ya kale yamepita. Unafanywa mpya.
Rudisha ujasiri wako na ufurahie kila baraka za Mungu!

**TAMKO LA KINABII**
Mimi ni kiumbe kipya katika Yesu Kristo! Mambo yangu mabaya yaliyopita yanafutwa kwa uwezo wa Roho Mtakatifu. Sizuiliwi tena na udhaifu au kushindwa kwa mwanadamu. Ninayaendesha mambo kutokea kwenye ulimwengu wa juu!

**MAFUNZO ZAIDI**
Maombolezo 3:22-23

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Luka 2-3



Jumanne, Oktoba 28

# CHANZO CHA MAJIBU YAKO

**Kutoka 14:15**
**BWANA akamwambia Musa, Mbona unanililia mimi? Waambie wana wa Israeli waendelee mbele.**

Wana wa Israeli walikabili mkanganyiko wao mkuu; walizongwa na bahari mbele na kufuatiwa na Wamisri nyuma. Walifikiri kutoka Misri ndio ushindi, lakini waligundua kuwa adui hakuwa na huruma. Hata Nabii Musa alitaka jibu, lakini jibu la Mungu lilikuwa kali: "Mbona unanililia?" Mungu alikuwa wazi, hakuna haja ya kunililia; rudi nyuma na kurekebisha suala hilo. Jibu tayari liko kwako.

Kilichokuwa kweli kwa Musa ni kweli kwako: huu si wakati wa kumlilia Mungu ili kupata majibu. Ni wakati wa kutumia haki yako ya Ki-Ungu na kuleta mabadiliko katika maisha yako. Suluhisho la kweli tayari liko ndani yako, na Mungu amekupa uwezo wa kubadilisha hali yako. Fungua mdomo wako, tamka uzima, na uendelee kusonga mbele!

**TAMKO LA KINABII**
Kinywa changu ni kalamu ya mwandishi aliye tayari. Mimi ni mtoa suluhisho. Ninaamuru na kutangaza majibu kwa kila kitu ambacho kimeunganishwa kwangu na familia yangu katika Jina la Yesu! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Luka 10:19

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Luka 4:1-6:26



Jumatano, Oktoba 29

# NJE YA KAWAIDA

**1 Mambo ya Nyakati 4:9-10**
**Naye Yabesi alikuwa mwenye heshima kuliko nduguze; na mamaye akamwita jina lake Yabesi, akisema, Kwa sababu nalimzaa kwa huzuni…**

Ulimwengu una ufafanuzi wake wa “kawaida”, kiwango ambacho wao hufafanua jinsi mambo yanaweza kutokea au yanapaswa kuwa. Kitu cha ajabu kinapotokea, kinaandikwa katika Kitabu cha Rekodi cha Guinness. Ukoo wa Yabesi ulifuata muundo wa “kawaida” unaotabirika: kizazi baada ya kizazi kikazaa kijacho. Hakuna kilichotokea, mpaka Yabesi. Alikataa kufuata kawaida na akathubutu kumwomba Mungu kumzidishia hozi yake. Kwa sababu hii, Biblia inasema alikuwa mwenye heshima zaidi kuliko ndugu zake.

Ninakuhimiza leo kuachana na kawaida. Unaweza kuzaliwa katika familia moja na jamaa zako, lakini hatima yako ni tofauti. Mafanikio yako yatakuwa ya kwanza kati ya ndugu zako. Mungu anakunyakua kutoka kwenye mzunguko wa ukawaida kwa Jina la Yesu!

**TAMKO LA KINABII**
Mimi si wa kawaida! Nitaishi zaidi ya matarajio ya ulimwengu. Kwa uwezo wa Roho Mtakatifu, ninavunja kila kikomo cha kipepo katika Jina la Yesu. Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Danieli 1:20

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Luka 6:27-8:25



Alhamisi, Oktoba 30

# AGENDA YA UFALME

**2 Mambo ya Nyakati 1:10 (NIV)**
**Basi sasa nipe hekima na maarifa, nijue kutoka na kuingia mbele ya watu hawa; kwa kuwa ni nani awezaye kuwahukumu watu wako hawa walio wengi?**

Watu wengi hukosa baraka za Mungu kwa sababu ya dhamira za maombi yao. Mungu hufadhili, hulinda, na kuendeleza ajenda yake. Unapoomba gari jipya au nyumba kubwa, dhamira yako nini? Je, ni kwa ajili ya marafiki zako kuona au kujionyesha karibu na ujirani wako?

Sulemani aliomba ufahamu, si ili kusifiwa kama mtu hodari wa wakati wake, bali kuchunga watu wa Mungu kwa usahihi. Kusudi lake lilikuwa safi, na ombi lake lilikuwa na kusudi la Ufalme. Ndio maana Mungu alikubali na kumwongeza zaidi.

Mungu anatafuta mioyo inayotanguliza Ufalme wake. Nia yako inapolingana na kusudi Lake, unapata upendeleo wa Ki-Ungu. Haihusu ukubwa wa ombi lako lakini nia iliyo nyuma yake. Kwa hiyo kuanzia leo, hakikisha kila ombi unalomwomba Mungu limeambatanishwa na kusudi la Ufalme, hakika atakutimizia.

**TAMKO LA KINABII**
Ninavutia pesa kwa misheni. Sababu yangu ya kuwepo ni kumtumikia Mungu kwa kila kitu kilicho ndani yangu kwa Jina la Yesu. Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Zaburi 69:9

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Luka 8:26-10:16



Ijumaa, Oktoba 31

# SIKU YA THAWABU

**Wagalatia 6:9 (NIV)**
**Tena tusichoke katika kutenda mema; maana tutavuna kwa wakati wake, tusipozimia roho.**

Kumtumikia Mungu huja na thawabu iliyohakikishwa. Huduma inahusisha zaidi ya kuhubiri kutoka kwenye mimbari. Kutoa, kuimba katika kwaya, na chochote kinachofanywa kwa upendo nje ya ibada kwa Mungu hakitaenda bure. Neno la Mungu linatuambia tusichoke katika kutenda mema, maana thawabu itakuja. Hiyo ina maana kwamba inawezekana kuchoka. Wengine waliacha upesi sana, bila kujua walikuwa wamebakisha saa chache tu kabla ya malipo yao. Usiwe mmoja wao.

Fanya uamuzi wa kimakusudi wa kumtumikia Mungu kwa moyo wote. Thawabu yako ni hakika, sasa na katika uzima ujao. Usiruhusu changamoto za sasa zikukatishe tamaa, maana siku yako ya malipo inakuja. Ninaomba na kutabiri kwamba thawabu yako iko sasa, katika Jina la Yesu.

**TAMKO LA KINABII**
Moyo wangu umejikita kwenye njia ninayopaswa kufuata; Nitaendelea kumtumikia Mungu kwa moyo wote. Majira yangu ya malipo ni sasa katika Jina la Yesu. Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Warumi 2:6

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Luka 10:17-12:12



Jumamosi, Novemba 1

# NEEMA YA MUNGU NI ZAWADI, SI THAWABU

**Waefeso 3:7**
**..... nalifanywa mhudumu wake, kwa kadiri ya kipawa cha neema ya Mungu niliyopewa kwa kadiri ya utendaji na uweza wake.**

Neema ni upendeleo wa Mungu ambao haujaugharamia, wala kuustahili. Waefeso 2:8-9 inatangaza kwamba ni kwa neema tumeokolewa, si kwa matendo yetu (yale tunayofanya), lakini kwa sababu ya yale Kristo amefanya. Neema inatukumbusha kwamba upendo wa Mungu hautegemei utendaji. Inatufikia katika kushindwa kwetu na kutuinua katika kusudi la Mungu. Neema ya Mungu hutusamehe yaliyopita, hututia nguvu sasa, na kulinda maisha yetu yajayo.

Hatugharamii neema; tunaipokea. Tunapokubali neema ya Mungu, tunawekwa huru kutoka kwa aibu na kuwezeshwa kuishi kwa haki. Neema haitupi kibali cha kutenda dhambi; ni uwezeshaji wa kushinda. Kila siku ni fursa mpya ya kutembea katika neema. Sherehekea neema ya Mungu; ni upendo wake katika matendo.

**TAMKO LA KINABII**
Ninapokea neema ya Mungu ambayo imevutiwa kwangu kupitia kazi zilizokamilika za Kristo. Nimefunikwa kikamilifu chini ya neema ya Mungu. Chochote ninachofanya, ninashinda! Haleluya!

**MAFUNZO ZAIDI**
2 Wakorintho 3:5

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Luka 12:13-14:11



Jumapili, Novemba 2

# MUNGU ANALIPA UAMINIFU

**Waefeso 6:10**
**Hatimaye, mzidi kuwa hodari katika Bwana na katika uweza wa nguvu zake.**

Uaminifu hausahauliki kamwe kwa Mungu. ( Waebrania 6:10 ) inatuhakikishia kwamba Mungu si dhalimu; Hatasahau kazi yetu na upendo tulioonyesha. Hata wengine wanapopuuza jitihada zako, Mungu huona kila tendo la uaminifu.

Uaminifu unamaanisha kuendelea kujitoa kwa mapenzi ya Mungu, hata wakati ni ngumu. Uaminifu kupitia majaribu na changamoto huleta kuinuka kwa Ki-Ungu kunakokuweka juu ya wengine. Uaminifu sio wa kuvutia kila wakati, ni kuonekana, kuwa thabiti na kutii hata wakati hakuna mtu anayekupongeza. Hata hivyo, katika Ufalme wa Mungu, sifa hizo huongoza kwenye kuinuliwa kwa daima.

( Wagalatia 6:9 ) hututia moyo, “Tusichoke katika kutenda mema, kwa maana tutavuna kwa wakati wake.” Zawadi yako inaweza isije papo hapo, lakini imehakikishwa. Mbingu inatazama. Kaa kwenye njia. Amini wakati wa Mungu. Taabu yako katika Bwana haitakuwa bure kamwe.

**TAMKO LA KINABII**
Nimeazimia kubaki kwenye njia. Nitasonga mbele na kupambana hadi muujiza wangu udhihirike. Sitachoka wala sitakata tamaa sasa. Mimi ni mshindi, zaidi ya mshindi katika Jina la Yesu! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Warumi 2:7

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Luka 14:12-16:31



Jumatatu, Novemba 3

# NIMEUMBWA KWA MFANO WA MUNGU ILI KUTAWALA

**Ayubu 33:4**
**Roho wa Mungu ameniumba, na pumzi ya Mwenyezi hunipa uhai.**

Tangu mwanzo, Mungu alimuumba mwanadamu kwa kusudi na nguvu. (Mwanzo 1:26) inasema, “Na tumfanye mtu kwa mfano wetu… wakatawale.” Kufanywa kwa mfano wa Mungu ni uteuzi wa Ki-Mungu wa kutawala.

Mfano wa Mungu ndani yetu huakisi tabia yake, hekima, ubunifu, mamlaka, na haki. Hakutuumba tuwe wahanga bali washindi. Utawala ulikuwa ni agizo la awali la Mungu kwa wanadamu, na kusudi hilo bado liko. Kwa hiyo, wakili kwa uadilifu na ushawishi kwa ubora.

Anguko la mwanadamu halikufuta sura ya Mungu; liliipotosha. Lakini kupitia Kristo, tunarejeshwa, na utawala wetu umekombolewa (Warumi 5:17). Hukuumbwa kuishi kwa hofu, kushindwa, au hali ya ukawaida. Uliumbwa kuinuka, kujenga, kuongoza, na kuunda ulimwengu wako. Tembea katika utambulisho wako wa Ki-Ungu. Zungumza kwa mamlaka. Fanya maamuzi kwa kuungwa mkono na Mbingu. Roho wa Mungu ndani yako anarejesha utawala wako.

**TAMKO LA KINABII**
Nimeumbwa kwa mfano wa Mfalme. Ninaishi kama mwana wa mfalme; Ninatawala kwa hekima, natembea katika kusudi, na ushawishi kwa neema katika Jina la Yesu! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Zaburi 104:30

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Luka 17:1-19:27



Jumanne, Novemba 4

# MUNGU NI UPENDO, MFANO WETU MKUU

**Yohana 15:13**
**Hakuna aliye na upendo mwingi kuliko huu, wa mtu kuutoa uhai wake kwa ajili ya rafiki zake.**

Uwe na fahamu kwamba Mungu haonyeshi tu upendo, Yeye ni upendo. (1 Yohana 4:8) inasema, “Yeyote asiyependa, hakumjua Mungu, kwa sababu Mungu ni upendo.” Asili yake ndicho kipimo cha kweli cha upendo, si hisia za kibinadamu au wema unaochakaa. Msalabani, Mungu alionyesha tendo kuu la upendo: tulipokuwa tungali wenye dhambi, Kristo alikufa kwa ajili yetu (Warumi 5:8).

Upendo wa Ki-Mungu hutuinua juu ya chuki. Chuki hugawanya; upendo unaunganisha. Chuki huharibu; upendo hurejesha. Upendo wa Mungu unaweza kushinda moyo wenye giza zaidi na kuponya majeraha ya ndani kabisa. Tunapotembea katika upendo, tunamwakisi Yeye. ( 1 Yohana 4:20 ) hutukumbusha kwamba hatuwezi kudai kwamba tunampenda Mungu huku tukiwachukia wengine, upendo ni uthibitisho wa imani.

Mwaka unapokaribia mwisho, chagua kuruhusu upendo wa Mungu utiririke ndani yako, hata wakati mambo ni magumu.

**TAMKO LA KINABII**
Upendo wa Mungu ndani yangu una nguvu kuliko chuki yoyote inayonizunguka. Nimekita mizizi katika upendo wa Mungu, na ninashinda chuki kila wakati katika Jina kuu la Yesu. Bwana asifiwe. Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Isaya 53:10

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Luka 19:28-21:9



Jumatano, Novemba 5

# NIMEUMBWA KWA KUSUDI LA KIUNGU

**Wafilipi2:13**
**Kwa maana ndiye Mungu atendaye kazi ndani yenu, kutaka kwenu na kutenda kwenu kwa kulitimiza kusudi lake jema.**

Wewe si ajali; wewe ni uumbaji wa makusudi wa Mungu. Aliunda maisha yako, akikuchochea kwa shauku, akiongoza maamuzi yako, na kukutia nguvu katika changamoto.

Kusudi la Mungu halijafichwa; linagunduliwa kwa kutembea pamoja Naye, kutafuta mapenzi yake kupitia maombi, kusoma Neno, na kutii sauti yake. Musa alipata kusudi jangwani, Esta katika jumba la kifalme, na Daudi kwenye uwanja wa vita. Haijalishi uko wapi, Mungu anaweza kufunua kusudi lako. Huna haja ya kulivumbua; jisalimishe tu na ugundue.

Uliumbwa katika Kristo Yesu ufanye matendo mema yaliyotayarishwa kwa ajili yako (Waefeso 2:10). Kusudi lake kwa maisha yako ni kubwa kuliko kushindwa au kuchelewa kokote . Anakomboa kila njia na anafanya mambo yote kwa faida yako. Pata ukweli huu katika Mwaka wa Mvunja Minyororo!

**TAMKO LA KINABII**
Niliumbiwa kusudi; maisha yangu ni sehemu ya mpango wa Ki-Ungu wa Mungu, na atakamilisha kile Alichoanza ndani yangu Mwaka huu wa Mvunja Minyororo, katika Jina la Yesu. Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Warumi 8:28

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Luka 21:10-22:46



Alhamisi, Novemba 6

# MADHABAHU KAMA SEHEMU YA MAKUTANO

**1 Samweli 7:12**
**Ndipo, Samweli akatwaa jiwe na kulisimamisha kati ya Mispa na Sheni. Akaliita jina lake Eben-ezeri, akisema, Hata sasa BWANA ametusaidia.**

Madhabahu za kiroho ni mahali pa makutano na Mungu ambapo Mbingu hukutana na Dunia, na mwanadamu huwasiliana na Mungu. Katika Maandiko, madhabahu ziliashiria nyakati takatifu za agano na kutembelewa. Zaidi ya miundo ya kimwili, zinaashiria wakfu wa kiroho. Leo, tunajenga madhabahu za kiroho kupitia maombi, ibada, kufunga, na kujisalimisha, tukialika uwepo hai wa Mungu.

Madhabahu ni ukumbusho wa ahadi na uwepo wa Mungu. Kwa kuziweka katika nyumba zetu, mioyo, na mazoea yetu, tunatengeneza nafasi kwa Mungu kukaa na kutuongoza. Zinatumika kama vikumbusho, vinavyofanya upya imani yetu na nguvu za kiroho. Acha madhabahu yako iwe kona yako ya maombi, wakati wa kuabudu, na kujisalimisha kila siku, na uangalie nguvu za Mungu zikidhihirika katika maisha yako, ndoa, na fedha.

**TAMKO LA KINABII**
Katika mwaka huu wa Mvunja Minyororo, madhabahu yangu itanena kwa ajili yangu. Najua Mungu wangu atanihuisha madhabahuni kwa nguvu, kusudi, na amani. Bwana asifiwe! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Yoshua 4:7

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Luka 22:47-24:23



Ijumaa, Novemba 7

# IMANI HUMPENDEZA MUNGU

**Mwanzo 15:6**
**Akamwamini BWANA, naye akamhesabia jambo hili kuwa haki.**

Imani ndio msingi wa uhusiano wetu na Mungu. (Waebrania 11:6) inatangaza, “Pasipo imani haiwezekani kumpendeza Mungu. Imani inakwenda zaidi ya itikadi, ni uaminifu, utegemezi, na kujisalimisha kwenye mapenzi yake. Mungu haendeshwi na hisia au sifa bali imani. Tunapomtumaini Mungu kikamilifu, hata katika sintofahamu, tunaleta furaha kwenye moyo Wake. Imani inamheshimu Mungu kwa sababu inakubali tabia yake. Inasema, “Mungu, ninakutumaini Wewe, hata bila kuona matokeo.”

Imani hufungua milango ya miujiza. Yesu alisema mara nyingi, “Imani yako imekuponya.” Hakuhitaji ukamilifu, imani tu. Imani si kipofu; imekita mizizi katika uaminifu wa Mungu uliothibitishwa. Kumbuka alichofanya na acha hilo likuongezee ujasiri kwa yale yaliyo mbele yako. Iwe ni kupanda mbegu, kusali kwa ajili ya uponyaji, au kutafuta cheo, imani humletea Mungu heshima, na Mungu huheshimu imani.

**TAMKO LA KINABII**
Ninatamka Neno la Mungu, naamini ahadi Zake, na kuamini wakati Wake. Nina imani kwa Mungu mkuu. Ninaishi ili kumpendeza; kwa hiyo, ninaishi kwa imani. Haleluya! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Warumi 4:3

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Luka 24:24-53; Yohana 1:1-2:11



Jumamosi, Novemba 8

# YEHOVA RAFA

**Zaburi 103:3**
**Akusamehe maovu yako yote, Akuponya magonjwa yako yote.**

Mojawapo ya majina ya Mungu yenye kufariji zaidi ni Yehova Rapha, “Bwana aponyaye.” Uponyaji sio tu kile ambacho Mungu hufanya, ni vile Yeye alivyo. Uponyaji wa Mungu unaenea zaidi ya kimwili; Yeye huponya waliovunjika moyo ( Zaburi 147:3 ), hurejesha amani ya akili ( Isaya 26:3 ), na huponya majeraha ya kiroho kupitia msamaha. Anaponya hata mataifa. Uponyaji wake ni rahisi, kamili, na unapatikana kwa roho, nafsi, na mwili.

Msalaba wa Kristo ni ishara kuu ya uponyaji. (Isaya 53:5) inasema, “Kwa kupigwa kwake sisi tumepona.” Yesu alibeba magonjwa na uchungu wetu ili tuweze kuishi kwa utimilifu. Uponyaji unaweza kuwa wa papo hapo au wa taratibu, lakini daima unasukumwa na upendo na huruma. Wakati mwingine ni wa ndani na usiyoonekana, lakini haina maana kwamba hauna nguvu.

Tunapofunga mapazia kwenye Mwaka wa Mvunja Minyororo, mwamini Yehova Rapha. Nena Neno Lake na simama katika imani, kwa maana uponyaji hutiririka pale imani inapokua.

**TAMKO LA KINABII**
Ninatembea katika afya ya Ki-Ungu; Nguvu za uponyaji za Yehova Rapha hupenya kila uti wa nafsi yangu, sasa na sikuzote. Kwa hiyo, magonjwa yako mbali nami kwa Jina la Yesu. Amina!

**MAFUNZO ZAIDI**
Mwanzo 15:26

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Yohana 2:12-4:38



Jumapili, Novemba 9

# KUTOA HUAKISI MOYO WA MUNGU

**Hagai 2:8**
**Fedha ni yangu, na dhahabu ni mali yangu, asema BWANA wa majeshi.**

Kutoa huakisi asili ya Mungu. Maandiko yanasema, “Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa…” (Yohana 3:16). Msingi wa uhusiano wa Mungu nasi ni moyo wake wa ukarimu. Tunapotoa, iwe muda, talanta, au rasilimali, tunaakisi tabia Yake na kuendeleza misheni Yake ya upendo na ukombozi.

Mfalme Daudi alitambua ukweli huu, akisema, “…Vitu vyote vyatoka kwako, na katika vitu vyako mwenyewe tumekutolea” (1 Mambo ya Nyakati 29:14). Mtazamo huu hubadilisha mawazo yetu kutoka kwa umiliki hadi uwakili.

Kutoa hupangilia mioyo yetu na vipaumbele vya Mungu, huongeza utegemezi wetu kwa Mungu, na hufunua mahali ambapo ibada yetu iko (Mathayo 6:21). Kutoa kwenye makanisa, misheni, au wahitaji husaidia kujenga maisha, jumuiya, na mataifa. Kanisa linastawi kwa njia ya uaminifu wa watoaji kwa moyo mkunjufu wanaopanda katika makusudi ya Mungu kwa unyofu. Fanya kutoa kuwa maisha yako ya furaha.

**TAMKO LA KINABII**
Kutoa kwangu ni ushuhuda unaoonekana wa imani yangu kwa Mungu. Utoaji wangu humletea Mungu heshima, huwabariki wengine, na hunibadilisha kutoka ndani hadi nje! Mimi ni mtoaji wa mfululizo kwa ajili ya Ufalme! Bwana asifiwe! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Zaburi 24:1

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Yohana 4:39-6:51



Jumatatu, Novemba 10

# NGUVU YA MAOMBI YA KUDUMU

**Warumi 12:12**
**Kwa tumaini, mkifurahi; katika dhiki, mkisubiri; katika kusali, mkidumu;**

Mara nyingi nimesema kwamba “ibilisi” si jina la Shetani bali ni maelezo yake ya kazi. Maana yake ni mtu anayepiga tena na tena mpaka atoboe. Huko ni kuendelea. Vivyo hivyo, sala yenye kudumu huonyesha imani isiyoyumbayumba katika ahadi za Mungu. Yesu Kristo alishiriki mfano wa mjane mwenye bidii ili kututia moyo tuombe daima na tusikate tamaa (Luka 18:1).

Kudumu katika maombi hakuhusu kurudiarudia; ni kuhusu kutia nanga tumaini lako kwa Mungu. Anasikia kilio chako lakini mara nyingi hutumia ustahimilivu ili kuboresha tabia yako na kuimarisha imani yako Kwake.
Tunapodumu katika maombi, misuli yetu ya kiroho inaimarika. Mtazamo wetu unahamia kwenye mambo ya milele, na maombi yanakuwa zaidi kuhusu ushirika na Baba kuliko kupata majibu tu.

Paulo anasema, “Ombeni bila kukoma” (1 Wathesalonike 5:17). Mkao huu wa kudumu wa maombi hujenga uthabiti, huongeza ukaribu, na hutusaidia kutambua wakati Wake. Yafanye maombi ya kudumu yawe ushuhuda wako.

**TAMKO LA KINABII**
Sitawahi kuchanganya ukimya wa Mungu kwa kutokuwepo kwake. Nitaendelea kuomba. Ninaunganisha maombi yangu kwenye mapenzi yake. Muujiza wangu hakika utatimia katika mwaka huu wa Mvunja Minyororo. Bwana asifiwe! Haleluya.

**MAFUNZO ZAIDI**
Wakolosai 4:2

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Yohana 6:52-8:20



Jumanne, Novemba 11

# UHARAKA WA KUVUNA NAFSI

**2 Wakorintho 6:2 (ESV)**
**...Tazama, wakati uliokubalika ndio sasa; tazama, siku ya wokovu ndiyo sasa.**

Kuvuna nafsi ni mapigo ya moyo wa Mungu. Yesu alikuja kutafuta na kuokoa waliopotea (Luka 19:10), nasi tumeitwa kuendeleza utume huo. Kila dakika ni muhimu; kila nafsi ni muhimu. Katika (Yohana 9:4), Yesu alisema, "Imetupasa kuzifanya kazi zake Yeye aliyenipeleka maadamu ni mchana..." Hatujui ni muda gani mtu anao au ni lini nafasi ya kushiriki Kristo inaweza kupita. Muda ni mfupi, na fursa hazitadumu milele, kwa hivyo tunahitaji kuchukua hatua sasa!

Kuvuna nafsi si kwa wahubiri pekee. Kila Mkristo ni shahidi (Matendo 1:8). Iwe kazini, nyumbani, au barabarani, unabeba ujumbe wa Habari Njema. Kila mkutaniko unaweza kuwa miadi ya Ki-Ungu na Yesu. Haihusu kuwa na majibu yote; bali ni kuhusu kushirikisha kile Yesu amefanya. Unapofungua kinywa chako kwa imani, Roho Mtakatifu hutia nguvu maneno yako. Kwa hiyo, sema tu kuhusu Yesu!

**TAMKO LA KINABII**
Sitachelewa tena, kwa maana najua kwamba utiifu wangu huchochea sherehe Mbinguni. Leo, ninaamua kukufanya kuvuna nafsi kama misheni yangu binafsi katika Jina la Yesu! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Isaya 55:6

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Yohana 8:21-10:18



Jumatano, Novemba 12

# KUMFURAHIA MUNGU KWA NJIA YA FARAGHA

**Wakolosai 3:10**
**mkivaa utu mpya, unaofanywa upya upate ufahamu sawasawa na mfano wake yeye aliyeuumba;**

Uzoefu kamili na Mungu huanza na faragha, si tu kumjua Yeye bali kumjua Yeye binafsi. ( Yakobo 4:8 ) inasema, “Mkaribieni Mungu naye atawakaribia ninyi. Mungu anatafuta uhusiano, si dini. Daudi alielewa hili. Hakutamani tu baraka bali ushirika na Yule ambaye alikuwa na sura aliyokuwa nayo.

Katika faragha, tunapata upendo, amani, na mwongozo wa Mungu. Tunasikia minong’ono Yake, tunajifunza moyo Wake, na kutembea katika hatua na Roho Wake. Hii si ya wachache waliochaguliwa, ni kwa yeyote anayemtafuta. Yesu mara nyingi alijitenga na kuomba, akionyesha mfano wa nguvu ya ushirika wa faragha (Luka 5:16). Kadiri ukaribu wako unavyoongezeka, ndivyo utambulisho wako na madhumuni yako yanavyoongezeka.
Mungu wa ulimwengu anatamani sana kutembea nawe kila siku. Sogea karibu na ufurahie uwepo Wake katika maisha yako, familia, na mahusiano.

**TAMKO LA KINABII**
Sitaridhika na dini ya mbali. Ninaingia kwenye uhusiano wa kina na Baba yangu. Ninatanguliza maombi, kuabudu, na kutafakari Neno Lake, sasa na siku zote, katika Jina la Yesu. Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Waefeso 4:22-24

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Yohana 10:19-12:11



Alhamisi, Novemba 13

# NENO LA MUNGU HALIBADILIKI NA LINATUMAINIKA

**Isaya 40:8**
**Majani hunyauka, ua lanyauka, bali neno la Mungu wetu litasimama milele.**

Katika ulimwengu wa maadili yanayobadilika-badilika na mifumo isiyo imara, Neno la Mungu hubaki imara na halibadiliki. Kuamini Neno Lake kunamaanisha kuweka maisha yako kwenye msingi wa milele ambao haushindwi kamwe.

Maisha yanapokosa uhakika, ahadi za Mungu hutoa uhakikisho. (Hesabu 23:19) inasema, “Mungu si mtu, aseme uwongo.... Iwapo amesema hatalitenda? Iwapo amenena hatalifikiliza?” Kila neno kutoka kwa Mungu ni safi, kweli, na la kutegemewa.

Biblia si kitabu cha kihistoria tu; ni hai na kinaishi (Waebrania 4:12). Tunaposoma na kutafakari juu yake, imani yetu inaimarishwa, akili zetu zinafanywa upya, na mioyo yetu inafarijiwa. Kuliamini Neno la Mungu hupatanisha matendo yetu na kweli yake. Inaleta amani katika machafuko na uwazi katika mkanganyiko. Tunapotembea kwa maagizo Yake, tunafurahia uaminifu Wake moja kwa moja.

**TAMKO LA KINABII**
Bila kujali dhoruba ninazokabiliana nazo, Neno la Mungu linabaki kuwa kimbilio salama na hakika kwangu. Nimejenga maisha yangu juu yake, naamini; kwa hiyo, ninatangaza, na sitatikisika kamwe katika Jina la Yesu. Amina!

**MAFUNZO ZAIDI**
Isaya 55:11

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Yohana 12:12-14:11




Ijumaa, Novemba 14

# IBADA NI UONESHO WA UPENDO

**Zaburi 150:6**
**Kila mwenye pumzi na amsifu BWANA. Haleluya.**

Kuabudu ni mwitikio wa moyo kwa ukuu na wema wa Mungu. Ibada ya kweli inabubujika kutoka kwa moyo uliozidiwa na jinsi Mungu alivyo. Si wimbo tu au tambiko la Jumapili bali ni mkao unaoendelea wa upendo wa uchaji na kujitoa. Kuabudu ni mtindo wa maisha! Fanya hii iwe kweli kwako na kwa familia yako.

Kuabudu hutuleta karibu na Mungu na kumleta Mungu karibu nasi. Katika ukaribu huo wa Ki-Ungu, tunapata nguvu, amani, na furaha. Ibada huhamisha mtazamo wetu kutoka kwenye matatizo hadi kwa ukuu wa Mpaji wetu. Pia inaalika uwepo wa Mungu kwa njia inayoweza kushikika. Tunapoabudu, tunatengeneza kiti cha enzi cha Mungu kutawala kila eneo la maisha yetu.

Hebu kila kitu unachofanya katika Mwaka huu wa Mvunja Minyororo kiwe tendo la ibada. Anastahili, si tu Jumapili, lakini kila siku ya maisha yako!

**TAMKO LA KINABII**
Nitamwabudu Mfalme wangu. Iwe katika wimbo, huduma, utoaji, au maombi, ibada yangu ni sadaka takatifu inayogusa Mbingu. Haleluya!

**MAFUNZO ZAIDI**
Zaburi 34:1; Isaya 43:21

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Yohana 14:12-17:13



Jumamosi, Novemba 15

# KRISTO ATARUDI HAKIKA

**Ufunuo 22:12**
**Tazama, naja upesi, na Ujira wangu u pamoja nami, kumlipa kila mtu kama kazi yake ilivyo.**

Nimezungumza mara nyingi juu ya unyakuo kwa sababu kurudi kwa Kristo ni ahadi ya uhakika. (Matendo 1:11) inatangaza, “Huyu Yesu aliyechukuliwa kutoka kwenu kwenda juu mbinguni, atakuja….” Kurudi kwake sio swali la ikiwa bali la lini. Yesu aliwahakikishia wanafunzi wake, “Nitakuja tena niwakaribishe kwangu; ili nilipo mimi, nanyi muwepo” (Yohana 14:3). Ahadi hiyo huleta faraja katika ulimwengu uliojaa misukosuko.

Kwa waaminifu, kurudi kwa Yesu hakupaswi kuogopwa, ni tumaini letu lenye baraka. Kuja kwake huleta thawabu, urejesho, na haki. Kila kosa litarekebishwa, na wale waliomwamini watatawala kwa utukufu. Hadi wakati huo, ni lazima tuendelee kuwa macho na waaminifu. (Mathayo 24:44) hutukumbusha kuwa tayari.

Mfalme anarudi. Na ukutwe ukiwa mwaminifu atakapotokea.

**TAMKO LA KINABII**
Nitaishi kila siku ya maisha yangu nikiwa na umilele akilini. Chaguzi zangu, mawazo, na matendo yangu yataakisi utayari wangu, kwani najua Yesu Kristo anakuja tena! Haleluya!

**MAFUNZO ZAIDI**
Warumi 2:6

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Yohana 17:14-19:42



Jumapili, Novemba 16

# IMANI HUSHAMIRI KATIKA USHIRIKA

**1 Wathesalonike 5:11**
**Basi farijianeni na kujengana kila mtu na mwenzake, vile vile kama mnavyofanya.**

Kuhudhuria kanisa sio tu utaratibu; ni nidhamu ya kiroho inayoimarisha imani yetu. (Warumi 10:17) inasema, "Imani chanzo chake ni kusikia, na kusikia huja kwa Neno la Mungu." Kila mkusanyiko huleta mafundisho mapya ambayo hujenga na kurutubisha imani yetu katika Kristo. Kanisa ni mahali ambapo Mungu huzungumza, huponya, na kukujenga. Inatukumbusha kuwa hatuko peke yetu. ( Waebrania 10:25 ) inahimiza, "Wala tusiache kukusanyika pamoja... bali tuonyane, na kuzidi kufanya hivyo kwa kadiri mwonavyo siku ile kuwa inakaribia."

Kusikia Neno la Mungu kila wakati hutusaidia kusimama imara katika nyakati ngumu. Jumbe tunazosikia, shuhuda tunazoshuhudia, na maombi ya ushirika hutuimarisha kiroho na kihisia. Kuhudhuria kanisani hututia nanga katika ukweli, hutukumbusha ahadi za Mungu na kutuhamasisha kukua katika haki. Imani haistawi kwa kujitenga; inastawi katika ushirika.
Tangaza kupenda kwako uwepo wa Mungu na kujidhatiti kwenye ukuaji wa kiroho, nenda kanisani.

**TAMKO LA KINABII**
Kuhudhuria kwangu kanisani ni sehemu isiyoweza kujadiliwa ya maisha yangu. Ninaenda kanisani kwa dhati, nikiwa tayari kufurahia nguvu zisizo za kawaida za Mungu katika Jina kuu la Yesu. Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Waebrania 3:13

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Yohana 20-21; Matendo 1:1-2:13



Jumatatu, Novemba 17

# ALAMA ZA DHABIHU

**1 Petro 2:5**
**Ninyi nanyi, kama mawe yaliyo hai, mmejengwa mwe nyumba ya Roho, ukuhani mtakatifu, mtoe dhabihu za roho, zinazokubaliwa na Mungu kwa njia ya Yesu Kristo.**

Madhabahu za kiroho huashiria dhabihu, mahali ambapo kitu cha thamani kinatolewa ili kumheshimu Mungu. Katika nyakati za Agano la Kale, madhabahu zilijengwa kwa ajili ya sadaka za kuteketezwa zikiashiria ibada, toba, na ibada. Leo, tumeitwa kuwa dhabihu zilizo hai (Warumi 12:1).

Ibada yako, shukrani, na muda unaotumia kuendeleza ajenda ya Mungu huugusa moyo Wake, ukijenga madhabahu inayochochea mwitikio wa Ki-Ungu. Kusalimisha faraja yako, kiburi, wakati, au rasilimali huonyesha uaminifu na heshima. Mfalme Daudi alisema, “Sitamtolea Bwana kitu kisichonigharimu” (2 Samweli 24:24). Madhabahu za kweli zinadai dhabihu ya maana.

Utiifu wetu wa kila siku, kuchagua kusamehe, kutumikia, au kutoa, pia ni sadaka yenye harufu nzuri. Tunaweka vipande vya nyama yetu juu ya madhabahu. Kila tendo linasema, “Si mapenzi yangu, bali Yako yatimizwe.”

**TAMKO LA KINABII**
Nitaishi maisha yangu kama dhabihu iliyo hai, na najua moto kutoka mbinguni utawaka katika mifupa yangu. Sadaka ninayomtolea Mungu inarudi na baraka na mafanikio. Bwana asifiwe. Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
1 Wakorintho 3:16-17

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Matendo 2:14-4:37



Jumanne, Novemba 18

# IMANI HUISHINDA HOFU

**Wafilipi4:13**
**Nayaweza mambo yote katika yeye anitiaye nguvu .**

Hofu ni ya asili, lakini imani ni ya Ki-Ungu. Hofu inapooza, lakini imani inasukuma. Maisha yanapokosa uhakika, tunachagua imani, si kwa kupuuza hofu, bali kwa kumtumaini Mungu zaidi ya tatizo. (Isaya 41:10) inasema, "Usiogope, kwa maana mimi ni pamoja nawe ... nitakutia nguvu na kukusaidia." Imani inaamini kwamba Mungu yupo, ana nguvu, na anaweza.

Daudi alikabiliana na Goliathi kwa imani. Wakati wengine wakitetemeka, Daudi aliamini. Yesu mara nyingi alisema, "Usiogope, amini tu." Imani hunyamazisha hofu kwa sababu inategemea ahadi za Mungu. Hofu inasema, "Vipi ikiwa?" Imani inasema, "Hata kama, Mungu bado ni mwema!" Petro alipotembea juu ya maji, imani ilimfanya aelee; hofu ilimfanya kuzama.

Weka macho yako kwa Yesu, na hofu itapoteza mshiko wake. Imani hukua kwa kusikia na kutafakari Neno la Mungu. Kadiri unavyomjua zaidi, ndivyo hofu inavyopungua!

**TAMKO LA KINABII**
Ninazungumza imani, nawaza imani, na kuishi imani. Hofu inaweza kubisha, lakini ninatumia imani kuijibu. Maana najua Mungu hajanipa roho ya woga bali ya nguvu, upendo na akili timamu katika Jina la Yesu! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Yoshua 1:9

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Matendo 5:1-7:29



Jumatano, Novemba 19

# KUTOA HUFUNGUA BARAKA ZA KIUNGU

**Mithali 19:17**
**Amhurumiaye maskini humkopesha Bwana; naye atamlipa kwa tendo lake jema.**

Kutoa ni kanuni ya kiroho inayofungua baraka za Ki-Ungu. Katika (Luka 6:38), Yesu anafundisha, "Wapeni watu vitu, nanyi mtapewa..." Tunapotoa bure, tunajiweka katika nafasi ya kupokea kwa wingi. Kutoa hakupaswi kuwa kwa ajili ya kupokea tu, lakini Mungu huitia ukarimu kwa mioyo ya ukarimu. Unapotoa kwenye miradi ya Mungu na kuwa sehemu yako, milango inafunguka kwa njia isiyo ya kawaida na kukuinua hadi viwango vipya vya ongezeko.

Baraka inayokufuata sio ya kifedha kila wakati. Inaweza kuja kama amani, ruzuku, fursa, au ulinzi. Hata mjane aliyetoa sarafu mbili ndogo alimvutia Yesu kwa sababu alitoa vyote alivyokuwa navyo (Marko 12:41–44). Mungu anathamini moyo ulio nyuma ya sadaka kuliko kiasi cha sadaka. Kutoa hubadilisha mtazamo wetu kutoka kwenye uhaba hadi kwenye utele na hutukumbusha kwamba Mungu, si kazi au akaunti ya benki - ndiye chanzo chetu. Toa na utangaze imani yako katika upaji wa Mwenyezi Mungu.

**TAMKO LA KINABII**
Utoaji wangu wa uaminifu humletea Mungu heshima na huamsha baraka za kiroho maishani mwangu. Utoaji wangu kamwe sio hasara bali ni uwekezaji. Nitavuna marejeo ya milele na ya duniani kwa Jina la Yesu! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
2 Wakorintho 9:6-7

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Matendo 7:30-9:22



Alhamisi, Novemba 20

# UPONYAJI NI RAHISI

**Yohana 6:2**
**Na mkutanao mkuu wakamfuata, kwa sababu waliona ishara alizowafanyia wagonjwa.**

Kila mahali Yesu alipoenda, uponyaji ulifuata. Uponyaji haukuwa wa kimatukio; ilikuwa muhimili wa huduma Yake. (Mathayo 4:23) inasema Yesu alizunguka Galilaya akiponya kila homa na magonjwa miongoni mwa watu. Haya hayakuwa tu kudhihirisha uwezo bali kudhihirisha huruma ya Mungu. Yesu alifungua macho ya vipofu, alifufua wafu, na kuponya umati. Miujiza yake ni matendo ya huruma, inayoonyesha kwamba Mungu anajali sana kuteseka kwa wanadamu.

Kwa neema yake, Mungu alitupa nguvu zake za uponyaji. Katika huduma hii, tumeona miujiza isiyo na idadi. Uponyaji ni rahisi unapofanywa kwa imani katika Jina Lake!
Mwanamke aliyetokwa na damu aligusa vazi la Yesu na akapona mara moja. Hadithi yake inatukumbusha kwamba imani inapofikia, Mungu hujibu. Yesu hakuwahi kumkataa yeyote aliyekuja kwa imani. (Waebrania 13:8) inasema Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo na hata milele. Alichofanya wakati huo, bado anafanya sasa.

**TAMKO LA KINABII**
Ninaamuru na kutangaza leo kwamba kila maumivu yameondolewa kutoka kwenye maisha yangu. Kama mtoto wa Mungu, mwili wangu ni hekalu la Roho Mtakatifu; kwa hiyo, nakataa kuwa mgonjwa! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Mathayo 14:14

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Matendo 9:23-11:30



Ijumaa, Novemba 21

# AMRI ILIYO KUU

**Mithali 10:12**
**Kuchukiana huondokesha fitina; Bali kupendana husitiri makosa yote .**

Alipoulizwa ni amri ipi iliyo kuu zaidi, Yesu alijibu, Mpende Bwana Mungu wako… na umpende jirani yako kama nafsi yako (Mathayo 22:37–39). Upendo sio hisia tu; ni amri. Inahitaji hatua, nia, na kujitoa. Upendo haudhuru. Unabadilisha hali ya hewa na kuleta amani, uponyaji, na umoja katika ulimwengu uliojaa migawanyiko.

Yesu hakufundisha upendo tu, bali aliuishi pia. Hata pale msalabani, aliomba, Baba, uwasamehe. Aliijibu chuki kwa upendo na anatuita sisi kufanya vivyo hivyo. Upendo wa Kristo ni mvumilivu, mwema, haukasiriki upesi, na hauweki kumbukumbu ya makosa. Ni thabiti, wa Ki-Ungu, na unatoka kwa Mungu pekee.

Roho Mtakatifu hutuwezesha kupenda zaidi ya uwezo wetu wenyewe. Upendo wake ni asili yetu. Hebu upendo huu uonekane katika maisha yako, familia, ndoa, biashara, na mahusiano. Acha upendo utiririke katika mwaka huu wa Mvunja Minyororo!

**TAMKO LA KINABII**
Ninachagua upendo badala ya chuki. Ninapotembea katika upendo, ninaakisi moyo wa Mungu, natimiza kusudi Lake, na kuonyesha aliye Mkuu zaidi anaishi ndani yangu, Mungu Mwenyewe! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
1 Petro 4:8

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Matendo 12-13



Jumamosi, Novemba 22

# MAOMBI, MAHALI PA KIMBILIO

**Wakolosai 4:2**
**Dumuni sana katika kuomba, mkikesha katika kuomba huku na kushukuru;**

Maisha bila shaka huleta dhoruba, kihisia, kimwili, na kiroho, lakini maombi ni kimbilio ambapo tunapata makao na nguvu. Mungu kwetu sisi ni kimbilio na nguvu, Msaada uonekanao tele wakati wa mateso (Zaburi 46:1). Kupitia maombi, tunaingia patakatifu pa Mungu na kupokea amani ambayo ulimwengu hauwezi kutoa. Hofu inapozidi, maombi hutuliza moyo. Wakati kuchanganyikiwa kunatawala, maombi huleta hakika. Mtunga-zaburi alitangaza, “nikizimia moyo, uniongoze juu ya mwamba nisioweza kuupanda” ( Zaburi 61:2 ). Mwamba huo ni Kristo, na maombi ndiyo njia inayotupeleka kwake kwa ujasiri.

Dhoruba za maisha zinapovuma, maombi hutupeleka kwa yule anayetuliza bahari. Mtwike yeye fadhaa zako zote kwa maana yeye hujishughulisha sana na mambo yako. Usirudi nyuma kwa woga, kimbilia kimbilio la maombi. Yeye ni mfukuza minong’ono.

**TAMKO LA KINABII**
Nitaomba, nikijua maombi ni itifaki ya Ki-Ungu inayoenda mbele yangu, ikipanga upya kila eneo ili kupata ushindi wangu. Sitaacha kamwe, kwa kuwa kupitia maombi, nitashinda, katika Jina la Yesu! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Waefeso 6:18

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Matendo 14:1-16:10



Jumapili, Novemba 23

# JUKUMU LETU

**Zaburi 96:3**
**Wahubirini mataifa utukufu wake, Na watu wote maajabu yake.**

Maagizo ya mwisho ya Yesu hayakuwa pendekezo bali amri, Agizo Kuu. “Enendeni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi…” Agizo hili la Ki-Ungu si la mitume, manabii, wachungaji, walimu au wainjilisti pekee; ni kwa kila Mkristo anayemwita Yesu Bwana. Utume Mkuu unatupa kusudi la imani yetu. Hatukuokoka ili tu kukaa kanisani bali kuwafikia waliopotea (Marko 16:15). Injili sio ushauri mzuri tu, ni habari njema ya neema ya Mungu inayobadilisha maisha.

Kuvuna nafsi kunahitaji nia. Mara nyingi hufanyika kupitia mazungumzo, mahusiano, na maisha ya kila siku. Yesu alikutana na watu kwenye visima, katika nyumba, na barabarani, akiwafikia siku zote, akiwa na upendo daima. Yesu aliahidi, “Mimi nipo pamoja nanyi siku zote.” Uwepo wake unatia nguvu utii wetu. Roho Mtakatifu hutayarisha mioyo, hutoa ujasiri, na kulithibitisha Neno. Hauko peke yako, endelea kushinda roho.

**TAMKO LA KINABII**
Kuvuna nafsi sio mzigo bali ni fursa kwangu. Ninapata kushirikiana na Mungu katika kuokoa roho kutoka gizani hadi kwenye Ufalme Wake wa ajabu wa nuru. Siko peke yangu; Ninavuna roho na Yesu! Haleluya! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
1 Mambo ya Nyakati 16:24

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Matendo 16:11-18:28



Jumatatu, Novemba 24

# UTII UNAJALISHA

**Zaburi 25:10**
**Njia zote za BWANA ni fadhili na kweli, kwao walishikao agano lake na shuhuda zake.**

Wengi wanatamani kukutana na Mungu, lakini ni wachache walio tayari kutii panapokuwa na ugumu. Hata hivyo, ni katika kujisalimisha nguvu zake zinafunuliwa. Utii ni lango la kuuona utimilifu wa Mungu. Kusikia Neno haitoshi. Ikiwa unataka matokeo, lazima uliishi. Utiifu hufungua ufunuo wa Ki-Ungu. Ibrahimu alimtii Mungu kwa kumtoa Isaka na akapata kondoo kwenye kichaka pamoja na ufunuo mpya wa Mungu kama Mpaji!

Utiifu hugeuza kawaida kuwa isiyo ya kawaida. Petro alitii agizo la Yesu la kushusha nyavu zake tena na kupata samaki wa kimuujiza. Mungu hukutana nasi kwa kiwango cha imani yetu. Hata wakati njia inaonekana kutokuwa wazi, utii hutuweka kwenye nafasi ya kukutana na Mungu. Mungu haitaji ufahamu, anahitaji kumuamini. Unapotembea katika utiifu, unapata ulinzi, upaji, na kusudi la Ki-Ungu. Chukua utii kwa uzito, huamsha baraka.

**TAMKO LA KINABII**
Nitamjua Mungu kikamilifu; Nitamtii kwa uaminifu. Katika utii wangu kwa Neno Lake, milango ya uhalisia wa Ki-Ungu itafunguka kwa ajili yangu. Bwana asifiwe! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Kutoka 19:5

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Matendo 19-20



Jumanne, Novemba 25

# AMANI NA UJASIRI KWA MUNGU

**Mathayo 7:24-25**
**Basi kila asikiaye hayo maneno yangu na kuyafanya, atafananishwa na mtu mwenye akili, aliyejenga nyumba yake juu ya mwamba...... isianguke kwa maana misingi yake imewekwa juu ya mwamba.**

Kutumaini Neno la Mungu huleta amani isiyo ya kawaida na uhakika usiotikisika. Nimeiona mara kwa mara, ahadi zake ni ngome ya mioyo na akili zetu katika nyakati zisizo na uhakika. Amani hutiririka tunapochagua kuamini kile ambacho Mungu anasema juu ya kile tunachoona au kuhisi. Hofu inapoingia, Neno la Mungu hutuhakikishia. "Usiogope" sio tu maneno ya kufariji, ni dhamana ya Ki-Ungu ya mafanikio na ushindi. Liamini Neno Lake, na imani yako itakua.

Kujiamini huja kwa kujua Neno la Mungu halirudi bure. Ikiwa Mungu amesema, atalitimiza. Yesu alitumia Neno kumnyamazisha adui. Vivyo hivyo, tunaposimama juu ya Neno, tunashinda mashaka, kuvunjika moyo, na udanganyifu. Acha Neno liwe nanga yako katika kila dhoruba.

**TAMKO LA KINABII**
Ninazungumza Neno la Mungu, ninaliamini, ninaliishi, na linakaa kwa wingi ndani yangu! Moyo wangu umejikita katika ukweli wa Mungu usiobadilika; kwa hivyo, nina amani na ujasiri usiotikisika! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Waefeso 6:17

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Matendo 21:1-23:25



Jumatano, Novemba 26

# KUABUDU HUBADILI MTAZAMO WAKO

**Zaburi 66:4**
**Nchi yote inakusujudia na kukuimbia; naam italiimbia jina lako.**

Ibada huhamisha mtazamo wetu kutoka kwenye mapambano ya kidunia hadi kwenye kweli za mbinguni. Maisha yanapotulemea, hutukumbusha enzi kuu na wema wa Mungu. Paulo na Sila, ingawa walipigwa na kufungwa, walisali na kumwimbia Mungu nyimbo. Ibada yao ilichochea uingiliaji kati wa Ki-Ungu; tetemeko la ardhi likavunja minyororo yao na kufungua milango ya gereza. Kuabudu sio tu jibu la baraka; ni tangazo la uaminifu wakati wa majaribu. Haipuuzi matatizo; inayaweka upya katika mwanga wa Mungu ni nani kwetu.

Tunapoinua macho yetu katika ibada, tunaacha kukuza matatizo na kuanza kumtukuza Bwana. Ibada huelekeza mwelekeo wetu kwenye chanzo chetu cha kweli cha msaada (Zaburi 121:1-2) na kuhamisha hali ya nje na mkao wetu wa ndani. Tunapoutazama utukufu wa Mungu, tunabadilishwa na kufanana naye. Sio wakati wa muziki tu, ni mkutaniko wa kubadilisha maisha!

**TAMKO LA KINABII**
Ninaamuru msimu mpya uanze ninapomwabudu Mungu. Ninapomwabudu Mungu, akili yangu inafanywa upya, moyo wangu unafanywa upya, na ninaikumbusha nafsi yangu kwamba Mungu bado yuko kwenye kiti cha enzi! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Zaburi 117:1

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Matendo 23:26-27:8




Alhamisi, Novemba 27

# KUSUDI LA MUNGU LINASHINDA

**1 Wakorintho 1:8**
**Ambaye atawathibitsha hata mwisho, ili msilaumiwe siku ile ya Bwana wetu Yesu Kristo.**

Maisha yamejaa misukosuko na mabadiliko, lakini kusudi la Mungu siku zote husimama (Mithali 19:21). Kile ambacho Mungu amekupangia hakiwezi kuzuiwa na mwanadamu, makosa, au hali. Kusudi lake hupitia kila nyakati, hupitia vyote baraka na vita. Safari ya Yusufu kutoka shimoni hadi ikulu ilionekana kuwa ya mkanganyiko lakini ilitimiza mpango wa Mungu wa kuokoa mataifa.

Kusudi haimaanishi maisha yasiyo na matatizo; ina maana maisha yenye maana. Mungu hutumia kila kitu, hata changamoto, kutimiza kusudi lake ndani yako. Unapohisi kupotea au kuchelewa, kumbuka Mungu hajasahau mpango wake. Yeye aliyeanza kazi njema ndani yako ataimaliza (Wafilipi 1:6). Usimuharakishe Mungu; Wakati wake ni kamili. Kusudi lake kwa maisha yako, biashara, familia, na fedha yako limetiwa muhuri Mbinguni; hakika Litashinda!

**TAMKO LA KINABII**
Najua Mungu wangu anaweza. Ninaamini katika uwezo Wake wa kunilinda sasa na siku zijazo. Ninaona mafanikio, na nitatembea katika hatima yangu na ushindi mkuu! Haleluya!

**MAFUNZO ZAIDI**
1 Wathesalonike 5:24

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Matendo 27:9-28:31; Warumi 1:1-15



Ijumaa, Novemba 28

# KUBWA KULIKO JANA YAKO

**Zaburi 103:12**
**Kama mashariki ilivyo mbali na magharibi, ndivyo alivyoweka dhambi zetu mbali nasi.**

Haijalishi jinsi maisha yako ya nyuma yalivyokuwa yamevunjika, neema ya Mungu inatoa mwanzo mpya. “Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita tazama! ( 2 Wakorintho 5:17 ). Neema inawezesha hili. Historia yako haiwezi kukuondolea sifa; neema inaandika upya hadithi yako. Maisha ya Paulo ni uthibitisho. Wakati mmoja akiwa mtesi wa Wakristo, alikumbana na neema kwenye njia ya kwenda Damasko na akawa chombo chenye nguvu cha Mungu.

Neema hufika gizani na kuleta nuru. Haipuuzi dhambi; inailipia (Warumi 3:24). Hakuna dhambi kubwa sana, hakuna kushindwa kwa kina sana, au majuto mazito ambayo neema haiwezi kulipia.

Neema ya Mungu hugeuza machafuko kuwa shuhuda na kushindwa kuwa majukwaa ya matumaini. Unapopokea neema Yake, hutatafsiriwa tena kwa yale uliyofanya bali kwa yale aliyokufanyia. Achana na yaliyopita na ukumbatie uhuru katika mwaka huu wa Mvunja Minyororo!

**TAMKO LA KINABII**
Ninatangaza kwa ujasiri kwamba neema inanipa rekodi safi na kesho tukufu. Haleluya!

**MAFUNZO ZAIDI**
Waebrania 4:16

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Warumi 1:16-5:11



Jumamosi, Novemba 29

# UTAWALA NI AMRI YA KIUNGU

**Ufunuo 5:10**
**Ukawafanya kuwa ufalme na makuhani kwa Mungu wetu; nao wanamiliki juu ya nchi.**

Utawala si uvumbuzi wa mwanadamu; ni jukumu ya kiungu. Katika (Mwanzo 1:28), Mungu aliwabariki Adamu na Hawa, akisema, “mtawale.” Hili halikuwa pendekezo bali amri kutoka kwa Muumba. Kuwa na mamlaka maana yake ni kutawala, kusimamia na kuongoza. Ni uwezo wa kushawishi, kujenga, na kuunda mazingira. Inaonyesha asili ya Mungu ndani yako kama msimamizi wa Dunia. Ishi kama mtu aliyekabidhiwa mamlaka ya kimungu.

Utawala si kwa faida ya ubinafsi bali ni kwa ajili ya kuendeleza Ufalme. Mungu anatutazamia kutawala kwa upendo, kuongoza katika haki, na kutumikia kwa mamlaka (Zaburi 8:6). Iwe katika biashara, elimu, huduma, au familia, umeitwa kuongoza. Hukuumbwa kujichanganya bali kusimama juu na kuwainua wengine ili utukufu wa Mungu uonekane Duniani kote!

**TAMKO LA KINABII**
Mimi si dhaifu; Nimepakwa mafuta kutawala. Akili yangu, mikono, na maneno yangu yana ushawishi. Uwepo wangu huleta utaratibu, ubora, na athari. Kwa hiyo, ninazungumza kwa ujasiri, nikijua Mbingu zinaniunga mkono kutawala nyanja yangu katika Jina kuu la Yesu! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
1 Petro 2:9

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Warumi 5:12-8:25



Jumapili, Novemba 30

# ISHARA ZA NYAKATI ZA MWISHO

**2 Tomotheo 3:1**
**This know also, that in the last days perilous times shall come. Lakini ufahamu neno hili, ya kuwa siku za mwisho kutakuwako nyakati za hatari.**

Yesu alitupa ishara za nyakati za mwisho ili kututayarisha. Katika ( Mathayo 24:6–8 ), Alizungumza juu ya vita, njaa, matetemeko ya ardhi, na manabii wa uongo, uchungu wa kuzaa ukiashiria nyakati. ( 2 Timotheo 3:1-5 ) hufafanua upotovu wa kimaadili kuongezeka: ubinafsi, majivuno, kutotii, na ukosefu wa utakatifu, mambo ambayo yanaonekana leo. Bado, usiogope; ishara hizi ni ukumbusho wa kukaa macho kiroho na kujikita katika Mungu.
Mathayo 24:14 inatuhakikishia kwamba licha ya machafuko hayo, Injili ya Ufalme bado itahubiriwa. Kama Wakristo, ni lazima tubaki tukiwa tumesimama imara katika Maandiko, tukiwa na bidii katika sala, na kuwa jasiri katika ushuhuda.
Usiogope ishara, wacha ziimarishe imani yako. Zinatukumbusha kwamba wakati ni mfupi, na nafsi lazima zifikiwe. Ishara sio mwisho; zinaelekeza kwenye kurudi kwa utukufu kwa Mwokozi wetu na mwanzo wa utukufu wa milele kwa waaminifu, kwa hiyo kuwa na shangwe katika mwaka huu wa Mvunja Minyororo!

**TAMKO LA KINABII**
Niko makini, niko macho, tayari, na nimechangamka kwa kuwa najua Mkombozi wangu anaishi. Mimi niko tayari kunyakuliwa mbali juu mawinguni katika unyakuo wa kwanza! Haleluya!

**MAFUNZO ZAIDI**
2 Petro 3:3

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Warumi 8:26-11:24



Jumatatu, Desemba 1

# USIWE NA S.A.D

**Yohana 14:26**
**Lakini huyo Msaidizi, huyo Roho Mtakatifu, ambaye Baba atampeleka kwa jina langu, atawafundisha yote, na kuwakumbusha yote niliyowaambia.**

Uchunguzi unaonyesha kwamba hisia za upweke na huzuni huhisiwa zaidi katika mwezi wa mwisho wa mwaka! Wanasaikolojia wamegundua kuwa mabadiliko ya msimu yanaweza kuathiri moja kwa moja ustawi wa kiakili wa mamilioni duniani kote, hali inayojulikana kama Matatizo ya Seasonal Affective Disorder (S.A.D). Kama mtoto wa Mungu, huwezi kuruhusu chochote katika ulimwengu huu kuamuru furaha na shangwe yako katika Bwana!

Upweke au kutokuwa na marafiki ni kwa wale ambao hawajui zawadi ambayo walipewa bila malipo mara tu walipompokea Kristo. Una Rafiki katika Roho Mtakatifu; Yeye ni Mfariji na Msimamizi wetu. Mungu amekupa mwongozo bora zaidi wa mazingira magumu ya maisha, si Rafiki tu, bali Yule anayekutia nguvu nyakati za uhitaji.

**TAMKO LA KINABII**
Siwezi kuwa peke yangu kamwe! Nina Rafiki katika Roho Mtakatifu. Ananifariji ninapohitaji. Hakuna kinachoweza, kwa vyovyote vile, kuniacha bila msaada! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
1 Wakorintho 6:19

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Warumi 11:25-15:33



Jumanne, Desemba 2

# MUUNDO WA KURUKA WA NDEGE WA SHEVIRONI

**Luka 22:32 (NIV)**
**Lakini nimekuombea wewe,ili imani yako isitindike, nawe utakapoongoka waimarishe ndugu zako.**

Ndege wakubwa wanaohama kama bukini, bata na bata maji mara nyingi huruka kwa muundo wa V au shevironi. Madhumuni ya mfumo wa kundi ni kuhifadhi nishati na kuboresha ufanisi wa angani. Miundo hii ya kuruka husawaidia ndege kufikia matokeo bora wanapokuwa wakipaa. Katika Ufalme wa Mungu, kusonga na kusudi na lengo lile lile kama ndugu na dada zako katika Bwana husitawisha misingi ya njia bora zaidi ya mwendo!

Maandiko yanatuonyesha kwamba kama watoto wa Mungu, tunaimarisha mwili wa Kristo kwa kusaidiana kwenye maombi. Kama vile ndege wanavyotumia nguvu ya umoja ili kukatiza pepo kali, Kanisa lenye umoja haliwezi kushindwa dhidi ya misukosuko ya mashambulizi ya adui. Leo, chagua kuwatia nguvu watoto wa Mungu katika maombi na uone matokeo ya matunda yakidhihirika katika maisha yako.

**TAMKO LA KINABII**
Ninawatia nguvu ndugu na dada zangu ninapotoa unabii! Sitaishi maisha ya kujiengua kutoka kwenye mwili wa Kristo au kuwa katika hatari ya kushambuliwa na adui. Umoja ni faida yangu! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
1 Wakorintho 1:10

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Warumi 16; 1Wakorintho 1:1-4:13



Jumatano, Desemba 3

# DARASA KATIKA VIPINDI

**1 Petro 2:2**
**Kama watoto wachanga waliozaliwa sasa yatamanini maziwa ya akili yasiyoghoshiwa, ili kwa hayo mpate kuukulia wokovu.**

Chukua muda kukumbuka siku zako za shule, kila wakati ulipomaliza mwaka, ulidhani kana kwamba umefikia kilele cha ufahamu wako, na kuingizwa kwenye kiwango kinachofuata. Tatizo la Wakristo wengi ni kwamba mara tu wanapofikia kiwango fulani cha ujuzi, wanakataa kutenga muda unaohitajika ili kukua hatua zaidi katika Mungu, na kutulia katika hisia potofu ya ukomavu.

Mtume Petro anatuambia kwamba kama vile watoto wachanga wanavyohitaji maziwa ili kukua na kuishi, kama mtoto wa Mungu, unapaswa kutamani maziwa ya Neno. Kama vile maziwa yanavyotia nguvu mifupa na kuwaimarisha watoto wachanga, Neno la Mungu hukutia nguvu na kukupa nguvu za kustahimili mashambulizi ya adui. Jifunze kutenga muda wa kusoma Maandiko Matakatifu, ukikuza akili na roho yako katika mchakato huo!

**TAMKO LA KINABII**
Nimetayarishwa kikamilifu na nguvu za Neno la Mungu lisiloweza kukosea, na hiyo inamaanisha nina uwezo wa kukwepa uvamizi wa shetani! Ninashinda leo! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
2 Petro 3:8

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: 1 Wakorintho 4:14-7:40



Alhamisi, Desemba 4

# KILICHOPO KWENYE MENU

**Zaburi 23:5 (NIV)**
**Waandaa meza mbele yangu, Machoni pa watesi wangu. Umenipaka mafuta kichwani pangu, na kikombe changu kinafurika.**

Wazo lisilo sahihi lililozoeleka sana katika Jumuiya ya Wakristo ni kwamba unyenyekevu humaanisha kuishi katika umaskini na ukata. Hata hivyo, Mungu anataka ufanikiwe! Biblia si maagizo ya maisha tu bali ni kanuni zilizothibitishwa zinazokuhakikishia mafanikio yako. Kwa kutumia kweli katika Neno lake, unapata nguvu sio tu kumshinda adui bali kustawi mbele yake!

Maandiko ya leo yanatoa taswira ya wazi: Mungu anakuandalia meza mbele ya adui zako! Kwenye menyu ni amani kamili, furaha, utele, uthibitisho. Meza ya Mungu haijajazwa na makombo, ni karamu iliyojaa neema! Na lililo bora zaidi? Ni Anaitayarisha mbele ya wale waliotarajia ushindwe! Umefanywa kuwa mshindi; kamwe usiruhusu chochote kishushe kiwango ambacho Mungu amekuwekea tayari!

**TAMKO LA KINABII**
Mungu ameniandalia meza mbele ya wenye mashaka nami. Neema, furaha, na ustawi viko kwenye menyu; Sipungukiwi chochote! Mimi ni mshindi katika Kristo! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Yohana 10:10

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: 1 Wakorintho 8:1-12:11



Ijumaa, Desemba 5

# UGUMU WA KUSIKIA

**Yohana 10:27**
**Kondoo wangu waisikia sauti yangu, nami nawajua, nao wanifuata;**

Ingawa,ni imani kwamba Mungu hutamani daima kuwasiliana na watoto Wake inakubalika kotekote, bila kujali dhehebu, rangi, au umri, Wakristo wengi wanaishi maisha yao yote bila kuwasiliana Naye. Je, hii ina maana kwamba maandiko yalipendekeza dhana ambayo haina uzito wa vitendo? Hapana! Hebu nielezee.

Katika audiolojia, vifaa vya kusikia husaidia watu ambao ni ngumu kusikia au viziwi. Vifaa hivi hutumia maikrofoni kunasa sauti za mazingira, amplifaya kuzichakata, na spika (kipokezi) ili kuicheza sauti iliyoimarishwa kwenye sikio.

Ingawa kiziwi amezingirwa na sauti, anahitaji kifaa cha kusaidia kusikia ili kuisikiliza na kuisikia. Vivyo hivyo, Mungu daima anazungumza, unahitaji tu Neno Lake kurekebisha masikio yako na roho yako ili kumsikia Yeye kwa uwazi! Zama ndani zaidi katika maandiko na uimarishe roho yako ili uwe msikivu zaidi wa sauti ya Mungu.

**TAMKO LA KINABII**
Mungu wangu bado anaongea! Ninayaelekeza vizuri masikio yangu sasa ili kumsikia Yeye kupitia matumizi ya Neno Lake. Siwezi kushindwa kamwe! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Mathayo 13:15

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: 1 Wakorintho 12:12-15:28



Jumamosi, Desemba 6

# MTU WA NENO

**Waefeso 6:17**
**Tena ipokeeni chapeo ya wokovu, na upanga wa Roho ambao ni Neno la Mungu.**

Pigano la ma panga ni mojawapo ya taaluma za umahili na umakini zaidi duniani, zinazotukuka na kuheshimiwa kwa zaidi ya milenia moja. Wakati Paulo, akiandikia kanisa la Efeso, anarejelea Neno la Mungu kama upanga wa Roho, anasisitiza usahihi wake, nguvu, na nia yake. Hii inadhihirisha ukweli wa kina wa kiroho. Changamoto zako nyingi za kila siku hutokana na kutolitumia Neno kama silaha dhidi ya shetani na majeshi yake.

Maandiko ni zaidi ya nukuu za kutia moyo kwenye malundo ya makaratasi ya ngozi; inabeba nguvu za kuangamiza pepo. Unaweza kulichalanga shambulio lolote la adui kwa uhakika na usahihi.

Kama mtoto wa Mungu, ni lazima utoe muda wa kutumia na kukua zaidi katika Neno la Mungu ili ubobee katika nidhamu yako; WEWE NI MTU WA NENO!

**TAMKO LA KINABII**
Mimi ni MTU WA NENO. Ninachukua Neno la Mungu pamoja nami kwenye vita. Nina uwezo wa kukatiza mipango ya shetani! Nitakuwa hakika na makini katika matumizi yangu ya Neno la Mungu leo! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Waebrania 4:12

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: 1 Wakorintho 15:29-16:24; 2 Wakorintho 1-2



Jumapili, Desemba 7

# LANGO LA KUPANDIA

**Mathayo 25:1-4**
**Ndipo Ufalme wa Mbinguni utakapofanana na wanawali kumi waliotwaa taa zao, wakatoka kwenda kumlaki bwana arusi. Watano wao walikuwa wapumbavu, na watano wenye busara. Wale waliokuwa wapumbavu walizitwaa taa zao, wasitwae na mafuta pamoja nao, bali wale wenye busara walitwaa mafuta katika vyombo vyao pamoja na taa zao.**

Wakristo kwa kawaida husema watakuwa kwenye 'safari ya kwanza' katika unyakuo. Hata hivyo, ni wachache wanaofikiria matokeo ya kuikosa safari hiyo. Hebu nielezee. Wakati wa kusafiri, unanunua tiketi ya mahali unakokwenda na wakati uliopangwa. Lakini usipofika lango la kupandia kwa wakati, unaweza kukosa safari ya ndege kabisa. Vile vile, kukosa unyakuo wa kwanza' kuna matokeo ya milele.

Katika mfano huu, Bwana Yesu anakazia uhitaji wa kuwa tayari kiroho, unaoonyeshwa na uchaguzi wa mabikira wa kuweka taa na mafuta yao tayari. Pia anasisitiza umuhimu wa uhusiano imara na Yeye. Daima kuwa tayari kwa unyakuo; tukutwe tukifanya kazi ya Mungu na kuleta matokeo katika Ufalme Wake!

**TAMKO LA KINABII**
NIKO TAYARI KWA UNYAKUO! Ninaelewa umuhimu wa kuwa kwenye safari ya kwanza ya kuelekea Mbinguni. Kwa wakati uliowekwa, nitakuwa tayari kwenye lango la bweni! Haleluya! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Mathayo 24:42-44

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: 2 Wakorintho 3-7



Jumatatu, Desemba 8

# SIWEZI KUONDOSHWA

**Matendo 20:24**
**Lakini siyahesabu maisha yangu kuwa kitu cha thamani, kama kuumaliza mwendo wangu, na huduma ile niliyopokea kwa Bwana Yesu, kuishuhudia Habari Njema ya neema ya Mungu.**

Je, utamtumikia Bwana bila kujali changamoto? Wakristo wengi wangesema “Ndiyo!” Hata hivyo matendo yao ya kila siku mara nyingi yanaonyesha kinyume. Mamilioni ya watu wamekataa kutumika katika Ufalme wa Mungu kwa sababu ya mashinikizo ya mitandao ya kijamii au maneno yenye kuvunja moyo kutoka kwa marika na familia.

Mstari wa leo unafafanua utiifu wa Mtume Paulo kwa Roho Mtakatifu alipokuwa akisafiri ilihali ndani, akijua kabisa mateso yanayomngoja. Licha ya dhiki zote katika huduma yake, alitangaza kwa ujasiri, hakuna hata moja ya mambo haya yanayoniyumbisha, wala sihesabu maisha yangu kuwa ya thamani kwangu. Alikataa kuyumbishwa hata mbele ya kifo! Kama mtoto wa Mungu, beba ujasiri huo huo na utangaze kazi iliyokamilika ya Kristo kwa ulimwengu, bila kujali matokeo.

**TAMKO LA KINABII**
Ninachagua kumfuata Kristo bila kujali upinzani! Hakuna shambulio la adui lenye uwezo wa kuniondosha. SIWEZI KUYUMBISHWA! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Yohana 15:18

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: 2 Wakorintho 8-12



Jumanne, Desemba 9

# MSAMAHA

**Waefeso 4:26**
**Mwe na hasira, ila msitende dhambi;**

Maandiko yanatuambia tusiliache jua litue tukiwa bado tuna hasira. Kwa hivyo ikiwa ni kosa lilitokea saa moja kabla ya jua kuchwa, unayo saa moja ya kusamehe na kusonga mbele! Je, nikiwasamehe na wakanikosea tena siku inayofuata? Samehe tena.

Katika (Mathayo 18:21-22), Yesu alisema tunapaswa kusamehe “saba mara sabini”, akiashiria msamaha usio na kikomo. Kimsingi, Alikuwa anaonyesha, “ni kwa kiasi gani utakosewa,” kwa sababu una uwezo wa kufanya hivyo.

Wakristo wengine hushikilia mambo kwa miongo kadhaa, wakikumbuka makosa yaliyopita kana kwamba yalitokea jana. Lakini ikiwa Mungu alikusamehe, ni nini kingeweza kuwa kikubwa sana kwako kusamehe? Unapozaliwa na Mungu, asili yako ni kusamehe. Omba msamaha kila wakati, au samehe, na kwa haraka, pia. Una hadi jua kuchwa!

**TAMKO LA KINABII**
Kuanzia leo, ninachagua kuwaona wengine jinsi Mungu anavyowaona. Hakuna mtu ambaye siwezi kusamehe na hakuna kosa ambalo siwezi kutoomba msamaha. Ninao uwezo wa kuwasamehe wengine makosa yao, na ninasamehe kwa moyo wote sasa hivi katika Jina la Yesu. Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Marko 11:25; 1 Yohana 1:7-10

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: 2 Wakorintho 13; Wagalatia 1:1-4:11




Jumatano, Desemba 10

# KUYAATHIRI MATAIFA

**Zaburi 2:8**
**Uniombe, nami nitakupa mataifa kuwa urithi wako, na miisho ya dunia kuwa milki yako.**

Mungu anaposema, “Nitakupa mataifa kuwa urithi wako,” Anazungumza kuhusu kuathiri roho za watu kwa Injili na haki ya Mungu. Mitume walifanya hivyo na kutupa mwongozo wa kufuata.
Paulo alipokuwa akihubiri Efeso, alikabili upinzani mkali, lakini haukuizuia Injili. Alipita taifa hadi taifa, akijua mataifa ndio urithi wake; hakukuwa na jinsi angeweza kupoteza. Biblia inatangaza hivi: “Hivyo ndivyo Neno la Bwana lilivyozidi na kushinda kwa nguvu” (Matendo 19:20). Ufunguo wa matokeo ya aina hii ni mzigo katika maombi.

Funga na kuwa na utungu katika maombi kwa ajili ya taifa lako, jiji, mji, shule, mahali pa kazi n.k., na hakika, Neno la Mungu litakua kwa nguvu ndani yake na kushinda. Wewe ndiye tumaini na suluhisho ambalo mataifa yanahitaji.

**TAMKO LA KINABII**
Nitahubiri Injili kwa ufanisi kwa waliopotea, nikiwatoa katika giza na kuwaingiza katika nuru ya ajabu ya Mungu. Neno linatawala katika mji wangu, taifa langu, na duniani kote katika Jina la Yesu! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
1 Tomotheo 2:1-2

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Wagalatia 4:12-6:18; Waefeso 1:1-14



Alhamisi, Desemba 11

# MAISHA YA KINA NDANI YA MUNGU

**Wakolosai 3:2-3**
**Yafikirini yaliyo juu, siyo yaliyo katika nchi. Kwa maana mlikufa, na uhai wenu umefichwa pamoja na Kristo katika Mungu.**

Wahubiri wengi husisitiza kujifisha nafsi yako, lakini maandiko ya leo yanasema wazi kwamba tayari tumekufa. Huna haja ya "kufa" tena ili kumtumikia Mungu na kuweka mawazo yako au mapenzi yako kwenye mambo ya kiroho. "Kwa maana mlikufa" inamaanisha wewe ni mtu mpya kabisa, aina mpya ya kiumbe ambacho hakijawahi kuwepo hapo awali.

Umekufa kwa ulimwengu, na ulimwengu umekufa kwako (Wagalatia 6:14). Tamani kuomba, kuabudu, kujifunza na kutafakari zaidi Neno. Haya ndiyo maisha yako mapya katika Kristo; kujitoa katika msimu huu wa mfungo. Weka shauku yako Kwake, juu ya Ufalme Wake wa mbinguni. Mpende kwa moyo wako wote na acha mambo ya Roho yawe ya maana zaidi kwako kuliko kitu kingine chochote. Hebu maisha haya ya kina zaidi ndani ya Kristo yawe ufahamu wako wa sasa kuanzia leo!

**TAMKO LA KINABII**
Ninatamka sasa kwamba nimeamshwa katika nguvu ndani yangu na kwa utambulisho wangu wa kweli katika Kristo. Ninaelekeza macho yangu kwenye uhalisia wa mbinguni na kuchagua kuingia kwenye kina zaidi katika Kristo katika Jina la Yesu! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Wakolosai 2:20

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Waefeso 1:15-5:14



Ijumaa, Desemba 12

# ATHARI ZA UKRISTO

**Mathayo 5:14**
**Ninyi ni nuru ya ulimwengu. Mji hauwezi kusitirika ukiwa juu ya mlima**

Katika nyakati hizi za mwisho, ulimwengu uliovunjika unahitaji Neno la Mungu kwa haraka. Wakristo ni mawakala wa mabadiliko, nuru inayotoa rangi za Mungu, kama maandiko ya leo yanavyoweka. Ulizaliwa ili uwe mvuto na jibu la kilio cha wahitaji. Kwa hiyo, weka utukufu ndani yako kazini; dhihirisha wema na ukamilifu wa Kristo ulio ndani ya roho yako.

Unapofunga na kuomba leo, kumbuka Ukristo ni mzuri tu kama alivyo Mkristo. Iwapo ungekuwa wewe pekee uliyejazwa na Roho Mtakatifu katika mji wako, jiji au nchi yako, bado kungekuwa na matokeo ya ajabu ya Injili mahali hapo. Uathiri ulimwengu wako; athiri maisha na Habari Njema, kwa kuwa hiyo ndiyo hamu ya Roho na mapenzi Yake kwenye maisha yako.

**TAMKO LA KINABII**
Ninatamka kwa mamlaka ya Roho kwamba mataifa yataathiriwa sana na Injili kadiri sauti za Wakristo zinavyozidi kuwa kubwa katika Jina la Yesu! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Habakuki 2:14

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Waefeso 5:15-6:24; Wafilipi1-2



Jumamosi, Desemba 13

# MAFANIKIO NI YANGU

**3 Yohana 1:2**
**Mpenzi, naomba ufanikiwe katika mambo yote na kuwa na afya yako, kama vile roho yako ifanikiwavyo.**

Mali mara nyingi huonekana kuwa viashiria vya mafanikio, ndiyo maana wengi hulinganisha mafanikio na pesa; lakini ni zaidi ya hapo.
Mafanikio ni mambo mengi. Ni uwezo wa kufanya kile unachotaka kufanya, kwenda unakotaka kwenda, na kuwa chochote unachotaka kuwa kwa utukufu wa Kristo! Ni uwezo wa kumpendeza Mungu, kutembea na Roho, na utukufu wake udhihirike katika maisha yako! Ni maisha yaliyojaa furaha na vicheko visivyoisha! Na zaidi ya mali, mafanikio ni uwezo wa kuwasaidia wengine wafanikiwe.

Biblia inasema Yusufu alikuwa mtu mwenye mafanikio (Mwanzo 39:2) kwa sababu aliifanya nyumba ya bwana wake Potifa kustawi. Umekusudiwa kufanikiwa sio tu kiroho, kiakili, kimwili, na kimwili, lakini pia kuwafanya wengine kufanikiwa. Haya ndio mafanikio ya kweli!

**TAMKO LA KINABII**
Ninatamka mafanikio yaje kwangu sasa. Neno la Mungu linatawala katika mwili wangu na fedha. Familia yangu na wengine watafanikiwa kwa sababu yangu katika Jina la Yesu! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Kumbukumbu la Torati 8:18; 2 Wakorintho 8:9

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Wafilipi3-4; Wakolosai 1



Jumapili, Desemba 14

# FAMILIA YANGU

**Yoshua 24:15**
**... lakini mimi na nyumba yangu tutatumikia BWANA.**

Yoshua alielewa nguvu ya familia. Karibu na mwisho wa maisha yake, aliwakusanya viongozi wa Israeli kwa ujumbe wa mwisho, akiwakumbusha juu ya baraka alizowapa Mungu ( Yoshua 24:1–14 ) na kuwahimiza kubaki waaminifu kwa Mungu. Katikati ya ujumbe wake, alitangaza maneno yasiyo na ukomo wa muda ambayo wengi hukariri na kuonyesha katika nyumba zao: “Lakini mimi na nyumba yangu tutamtumikia Bwana.”

Unaona jinsi Yoshua alivyoibinafsisha? “Lakini mimi.” Hatimaye, inakuja kumaanisha kwamba; Lazima uchague kumtumikia Bwana. Haitatokea kwa bahati mbaya, na haiwezi kurithiwa. Wengine wanaweza kupitisha urithi wa imani, lakini lazima uamue kuufanya kuwa wako.
Msimu huu wa sikukuu, fanya uamuzi wa kumtumikia Mungu kama familia. Ni zawadi kubwa zaidi unaweza kushiriki. Soma neno pamoja, ombeni pamoja na kukua pamoja. Ondoeni uovu wowote, fanyeni amani ninyi kwa ninyi na acha upendo uongoze. Anza leo!

**TAMKO LA KINABII**
Ninatabiri kwamba mimi na familia yangu tutamtumikia Mungu kwa moyo wote. Hakuna hata mmoja wetu atakayeachwa nyuma. Nyumba yetu ni ya Mungu katika Jina la Yesu! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Zaburi 133:1; Matendo 10:2

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Wakolosai 2-4; 1 Wathesalonike 1:1-2:12



Jumatatu, Desemba 15

# JITABILIE

**1 Tomotheo 1:18**
**Mwanangu Timotheo, nakukabidhi agizo hilo liwe akiba, kwa ajili ya maneno ya unabii yaliyotangulia juu yako, ili katika hayo uvipige vile vita vizuri.**

Biblia imejaa maneno ya baraka na unabii kuhusu maisha yako. Je, umevichukua kwa uzito? Umefanya nini na unabii wote uliosemwa juu yako, kujumuisha ule ulioandikwa kukuhusu katika Biblia? Wengine husema, “Sijapata mtu yeyote wa kunitabiria kuhusu maisha yangu” Basi jitabirie mwenyewe!

Mungu alisema kila Mkristo anapaswa kutamani karama ya unabii kwa sababu ni zawadi muhimu sana. Katika mstari wa leo, Timotheo anaambiwa apigane vita vizuri kwa unabii ulionenwa juu yake. Hiyo ina maana angeweza kuutumia kama silaha. Kwa kuwa hili ni Neno la Mungu, haliko kwa Timotheo tu; linatumika kwako pia. Katika Taifa la HabariNjema, sisi ni watu wa unabii, tumeundwa kwa unabii; unabii huja kiasili kwetu.

**TAMKO LA KINABII**
Ninatabiri kwamba kila Neno lililonenwa juu yangu litatimia licha ya vikwazo. Ninatamka moto uje na kuchoma kila kitu kinachonizuia sasa, katika Jina la Yesu! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Danieli 11:32b; 1 Wakorintho 14:39

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: 1 Wathesalonike 2:13-5:28; 2 Wathesalonike



Jumanne, Desemba 16

# AFYA YA KIMUNGU

**3 Yohana 1:2**
**Mpenzi, naomba ufanikiwe katika mambo yote na kuwa na afya yako, kama vile roho yako ifanikiwavyo.**

Mstari wa leo unasema, “Mpenzi, naomba ufanikiwe katika mambo yote na kuwa NA AFYA,” sio “...na UPONYWE.” Hiyo ina maana mpango wa Mungu kwa ajili yako ni afya ya Ki-Mungu! Hataki uteseke na maumivu ya kichwa, mafua, na homa; kusiwe na ugonjwa wa kisukari, shida ya tumbo, au masaa yasiyoisha katika ofisi ya daktari. Lililo bora kwake ni kutokuumwa hata kidogo!

Kuna maisha bora kuliko uponyaji. Mungu hataki uishi katika eneo la kuponywa ugonjwa mmoja au mwingine kila mara. Anakutaka ufikie mahali pa ushindi, ambapo huwi mgonjwa kamwe na kuelewa afya ya Ki-Ungu, ambayo ni kuu kuliko uponyaji wa Ki-Ungu. Wewe ni kiumbe kipya katika Kristo. Ugonjwa ni Agano la Kale sana! Ishi katika uhalisia wa afya ya Ki-Mngu kuanzia leo!

**TAMKO LA KINABII**
Afya ya Ki-Mngu ni urithi wangu niliopewa na Mungu. Kuanzia leo, ninatabiri kwamba ugonjwa hautanigusa; homa za aina yoyote, bakteria, au virusi hazitapatikana popote karibu na makazi yangu kwa Jina la Yesu! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Warumi 8:11; Isaya 33:24

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: 1 Timotheo 1-5



Jumatano, Desemba 17

# MAISHA MAREFU

**2 Tomotheo 1:10**
**...aliyebatili mauti, na kuufunua uzima na kutokuharibika, kwa ile Injili.**

Watu fulani katika Biblia waliishi zaidi ya miaka 900. Lakini kadiri dhambi ilipoongezeka, muda wa kuishi ulipungua sana (Mwanzo 6:3). Maandiko ya leo yanatuambia kwamba Bwana Yesu alishughulikia kikomo cha maisha marefu, ambacho ni dhambi. Kupitia dhabihu yake, alitoa wokovu kutoka kwenye dhambi na kufanya uzima wa milele uwezekane.

Kwa hivyo, hatupaswi kufa? Kwa msisitizo ndiyo! Tuna uwezo wa kuishi zaidi ya vifungo vya mipaka ya kidunia. Wengi wetu tutakuwa hai na kunyakuliwa kimwili wakati tarumbeta itakapolia. Kanisa lazima sasa lishike na kutembea katika nuru ya ukweli huu. Una uzima wa Mungu, uzima wa Ki-Ungu. Hauko chini ya ugonjwa au kifo! Wewe ni mshiriki wa asili ya Ki-Ungu ya Mungu. Ikiwa Mungu haugui wala hafi, huna sababu ya kukaa katika bonde la mauti!

**TAMKO LA KINABII**
Ninasimama imara katika Neno la Mungu, ambalo ni afya ya mwili wangu na uzima wa mifupa yangu. Ninapozungumza sasa, maneno yangu yanachochea kuachiliwa kwa nguvu za Ki-Mungu ambazo hutengeneza uwanja wa nguvu usiopenyeka kunizunguka, na kunipa maisha marefu katika Jina la Yesu! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Zaburi 91:16; Wathesalonike 4:16-17

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: 1 Tomotheo 6; 2 Tomotheo 1-4



Alhamisi, Desemba 18

# USHINDI NI WANGU

**Kutoka 17:11**
**Ikawa, Musa alipoinua mkono wake, Israeli walishinda, na alipoushusha mkono wake, Amaleki walishinda.**

Kanisani mara nyingi tunasema, “inua mikono yako,” iwe katika maombi, ibada au sifa. Kwa nini? Kwa sababu mikononi mwako kuna nguvu inayoleta ushindi. Paulo, akimwandikia Timotheo, alisema, “Basi nataka wanaume wasalishe kila mahali, huku wakiinua mikono iliyotakata…” (1 Timotheo 2:8).

Tazama kwa makini mstari wa leo. Katika vita dhidi ya Amaleki, Haruni na Huri walitambua kwamba ushindi wa Israeli ulihusishwa na mikono ya Musa kuinuliwa. Alipochoka, wakamketisha juu ya jiwe na kuinua mikono yake kila upande, wakaiinua mpaka Amaleki waliposhindwa. Kuinua mikono ni mbinu ya Roho kwa ushindi wako wa kudumu. Inaweza isilete maana, lakini inaleta imani! Ikiwa ilifanya kazi kwa Musa, itafanya kazi kwako unapoinua mikono yako na kudai ushindi wako leo!

**TAMKO LA KINABII**
Ninapoinua mikono yangu katika maombi, kila changamoto ninayokabiliana nayo leo tayari imeshindwa! Ninakiri ushindi katika kila jambo katika Jina la Yesu! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
1 Yohana 5:4; Zaburi 63:4

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Titus 1-3; Philemon 1; Waebrania 1:1-2:10



Ijumaa, Desemba 19

# ULIMWENGU WA HABARI NJEMA

**Warumi 8:14**
**Kwa kuwa wote wanaoongozwa na Roho wa Mungu, hao ndio wana wa Mungu.**

Maandiko ya leo yanahusu ukomavu wa kiroho. Inazungumza juu ya wana wa Mungu ambao wamekomaa kikamilifu, wale ambao hawatatenda isipokuwa wameongozwa na Roho Mtakatifu.
Kama mtu anayefuata maono ya Ulimwengu wa Habari Njema, jifunze kumfuata Roho katika Neno, kwa Neno, na kupitia Neno. Kamwe usifanye maamuzi makubwa katika maisha yako bila kushauriana Naye. Tumia muda kutafuta mwongozo wake; kuwa na subira mpaka uisikie sauti Yake, maneno Yake, katika roho yako, na kamwe usipingane na yale aliyosema katika Neno Lake. Huo ndio ukomavu.

Kuwa na Roho Mtakatifu kama GPS, ramani, na dira ya maisha yako kutakuhakikishia mahali pazuri tu katika maisha yako na Kanisa. Ubalozi wa Roho ni wewe, Ubalozi wa Roho wa Mungu. Ikiwa unaongozwa na Roho, Kanisa linaongozwa na Roho.

**TAMKO LA KINABII**
Kila tamko la kinywa changu, mwelekeo wa hatua zangu, na uamuzi ninaofanya unaongozwa na Roho wa Mungu. Ninabadilisha ulimwengu wangu na tawi la kanisa langu kuwa bora katika Jina la Yesu!

**MAFUNZO ZAIDI**
1 Petro 5:2-3; 1 Yohana 1:6-7

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Waebrania 2:11-6:20



Jumamosi, Desemba 20

# KUWAOMBEA VIONGOZI

**Warumi 15:30**
**Ndugu zangu, nawasihi Bwana Yesu Kristo, na kwa upendo wa Roho, jitahidini pamoja nami katika maombi yenu kwa ajili yangu mbele za Mungu;**

Katika barua zake zote, Mtume Paulo aliwahimiza watakatifu wamwombee, akijua maombi yao yalichochea ufanisi wa huduma yake, ukweli ambao bado unashika hadi leo. Kama Mkristo, umeitwa kuwaombea wale ambao Mungu ameweka juu yako, kwa ajili ya Bwana Yesu Kristo na kwa sababu unampenda Roho wa Mungu.

Ukiendelea kusoma, utaona kwamba maombi kama haya yanafaidisha sana mwili wa Kristo. Paulo alieleza jinsi yanavyonufaisha Ufalme hatimaye. Unapowaombea viongozi wako, nafsi zinavuna, maisha yanabadilishwa, na jina la Yesu linainuliwa. Kujua kwamba watakatifu wanawaombea kunatia moyo hata viongozi wa kanisa wateule zaidi. Wanasimama kidete na kwa ujasiri zaidi kwenye mstari wa mbele, wakijua umeinua mikono yao katika maombi. Hakikisha unafanya hivyo mara nyingi.

**TAMKO LA KINABII**
Ninatamka maisha marefu, afya ya Ki-Mungu, amani na furaha kwa wale walio katika uongozi! Ninatangaza kutiwa nguvu ya kufanya hata zaidi katika Ufalme ili roho zaidi zivunwe kwa Kristo katika Jina la Yesu! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Waefeso 6:19; Wakolosai 4:3

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Waebrania 7-10



Jumapili, Desemba 21

# OMBI LA MAOMBI YA MUNGU

**Mathayo 9:37-38**
**Ndipo alipowaambia wanafunzi wake… Basi mwombeni Bwana wa mavuno apele watenda kazi katika mavuno yake.**

Mungu mara chache huwa na hoja ya maombi, lakini hii ni mojawapo. Anapofanya hivyo, anafunua haja ya moyo wake, na kukupa fursa ya kushirikiana naye katika kutimiza kusudi lake duniani. Huyu ndiye Mungu yule yule aliyesema, “Kama ningekuwa na njaa, singekuambia” (Zaburi 50:12). Hata hivyo Anachukua muda kufanya ombi hili lijulikane. Hiyo inakuambia jinsi ilivyo muhimu.

Hitaji kuu la Baba yetu ni watenda kazi, wale walio tayari kwenda kuvuna mavuno ya roho zinazongoja kuokolewa. Msimu huu wa Krismasi ni fursa nzuri kwako kujibu ombi hili la maombi. Nafsi unazotakiwa kuzivuna tayari zimeandaliwa na zinangojea, kwa hivyo hakuna haja ya kuomba juu ya hilo. Kinachohitajika ni watenda kazi. Haya ni matakwa ya Mungu, yatimize sasa!

**TAMKO LA KINABII**
Ninatabiri kwamba mimi ni utimilifu wa ombi la maombi  ya Mungu, mtenda kazi mzuri kuleta mavuno makubwa ya nyakati za mwisho. Kila mtu ninayekutana naye ambaye hamjui Mungu atamgeukia leo na kuishi kwa ajili yake katika Jina la Yesu! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Yohana 4:35

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Waebrania 11-13



Jumatatu, Desemba 22

# YESU ALIFANYA

**Wakolosai 1:27**
**ambao Mungu alipenda kuwajulisha jinsi ulivyo utajiri wa utukufu wa siri hii katika Mataifa; nao ni Kristo ndani yenu, tumaini la utukufu.**

Mojawapo ya sababu kuu za kusherehekea Krismasi ni kwamba Yesu alitimiza kusudi lake! Yale aliyozaliwa kufanya, aliyafanya! Utukufu haleluya! Hebu fikiria matokeo yake kama hangekamilisha kazi Yake. Maisha yetu yangekuwa tupu na yasiyostahimilika bila tumaini. Lakini alikuja, akaishi, akafa, na kufufuka ili wewe na mimi tuweze kuishi kweli.

Zaidi ya mikusanyiko, chakula, muziki, na ushirika, Krismasi inamhusu Kristo, Yeye ni nani na kwa nini Alikuja. ( Mathayo 1:23 ) inasema, “Bikira atachukua mimba, naye atazaa mwana, nao watamwita jina lake Imanueli (maana yake “Mungu pamoja nasi”).” Mungu yu pamoja nasi; hatuko peke yetu! Muumba anaishi kati ya viumbe vyake, ni baraka iliyoje!

Krismasi hii, kumbuka: Alipata siku ya kuzaliwa, lakini tulipata zawadi! Hebu tusherehekee zawadi ambayo ni Kristo leo!

**TAMKO LA KINABII**
Nikiwa na Kristo ndani yangu, haiwezekani kushindwa! Utukufu wake utang’aa zaidi katika maisha yangu kuanzia leo, katika Jina la Yesu! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Yohana 1:14

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Yakobo 1:1-4:10



Jumanne, Desemba 23

# MAHALI PA UWEZA

**Waefeso 1:20-21**
**...Akamweka mkono wake wa kuume katika ulimwengu wa roho, juu sana kuliko ufalme wote, na mamlaka, na nguvu, na usultani, na kila jina litajwalo, wala si katika ulimwengu huu tu, bali katika ule ujao pia;**

Wengine husema, “Fulani ni mtu wa kuume kwangu,” kumaanisha wanawakilisha na kuzungumza kwa niaba yao. Vivyo hivyo, Biblia inaposema Yesu ameketi mkono wa kuume wa Mungu, ina maana ameshikilia kiti cha uweza, Mungu anatenda kazi kupitia Yeye.

Bwana Yesu anayo mamlaka isiyo na kifani juu ya vitu vyote; Jina Lake linasimama juu ya kila cheo, na utawala Wake unapita kila ngazi na uongozi wa mamlaka. Jambo bora zaidi ni kwamba wewe ni mshiriki wa mamlaka hii! Huyo ndiye Bwana Yesu Kristo tunayemsherehekea sasa, si mtoto mchanga kwenye hori! Mamlaka Yake hayajui mipaka, na wala Hana anayelingana naye. Haleluya! Leo, nenda nje ukijua una mamlaka kamili juu ya matukio ya siku hiyo.

**TAMKO LA KINABII**
Nimeketishwa mahali pa uweza na mamlaka kupitia Kristo! Kila mamlaka aliyonayo, ninayo. Nina nguvu nyingi sana na nimebarikiwa katika Jina la Yesu! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Waebrania 1:1-3

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Yakobo 4:11-5:20; 1 Petro 1:1-3:12



Jumatano, Desemba 24

# THIBITISHA UPENDO WAKO

**Waefeso 3:19**
**na kuujua upendo wa Kristo upitao ufahamu kwa jinsi ulivyo mwingi, mpate kutimilika kwa utimilifu wote wa Mungu.**

Wakati wa Krismasi, ni rahisi kusema “Nakupenda”, ni sehemu ya “roho ya Krismasi.” Lakini wengi wanachanganya kuvumiliana na upendo, wakidhani viko sawa. Katika Mambo ya Walawi 19:18, Biblia inasema, “Mpende jirani yako kama nafsi yako.” Neno “jirani” hapa linamaanisha wale walio karibu nawe, marafiki, familia, washiriki wa kanisa, sio tu majirani halisi. Lakini ni wangapi wanaoweza kusema kwa unyoofu wanawatendea wengine jinsi wanavyojitendea wenyewe?

Bwana Yesu alikuja na kudhihirisha upendo wa Mungu kwa njia ambayo ilikuwa tofauti. Alisema, “Hakuna aliye na upendo mwingi kuliko huu, wa mtu kuutoa uhai wake kwa ajili ya rafiki zake” (Yohana 15:13). Alituonyesha upendo kutoka kwenye mtazamo wa Mungu, na sio tu kwamba Alihubiri upendo huu, lakini pia aliuthibitisha. Krismasi hii, ifanye iwe hatua ya kuthibitisha kuwa unawapenda wengine.

**TAMKO LA KINABII**
Upendo wa Mungu umemiminwa ndani ya moyo wangu; kwa hivyo, kuwapenda wengine zaidi itakuwa rahisi kwangu. Nitaonyesha upendo huu hata zaidi Krismasi hii katika Jina la Yesu! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Wagalatia 2:20

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: 1 Petro 3:13-5:14; 2 Petro 1-2



Alhamisi, Desemba 25

# UJUMBE WA MALAIKA

**Luka 2:11-14**
**Maana leo katika mji wa Daudi amezaliwa kwa ajili yenu, Mwokozi, ndiye Kristo Bwana. … Mara walikuwapo pamoja na huyo malaika, wingi wa jeshi la mbinguni, wakimsifu Mungu, na kusema, Atukuzwe Mungu juu mbinguni, na duniani iwe amani kwa watu aliowaridhia.**

Ni ujumbe mzuri ulioje kupokea, siku ambayo kila kitu kilibadilika na kuwa bora kwako na mimi, haleluya! Yesu alizaliwa ili kutimiza mapenzi ya Baba, upendo wa Mungu uliodhihirishwa. Akawa Mwana-Kondoo wa dhabihu, akilipa gharama ya wokovu na kuwaleta wanadamu katika ushirika na Mungu.

Hebu fikiria Mwenyezi Mungu mjuzi wa yote, muweza wa yote, akiamua kutokuangalia ukiishi peke yako bali anatengeneza mpango mkuu wa kuishi nawe na ndani yako. Popote uendapo, chochote ufanyacho, Yeye yuko papo hapo pamoja nawe. Hii ndiyo hazina kuu inayotolewa kwa wanadamu. Sherehekea kuzaliwa kwake leo, ukijua ilikuletea nini.

Kheri ya Krismasi!

**TAMKO LA KINABII**
Ninatabiri kwamba siku zote za maisha yangu, sitasahau kiini cha kweli cha Krismasi. Nitasambaza ujumbe huu wa nia njema kwa kila mtu katika ulimwengu wangu. Asante, Bwana Yesu! Haleluya! Utukufu ni kwa Mungu. Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
2 Wakorintho 4:7

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: 2 Petro 3; 1 Yohana 1:1-3:12



Ijumaa, Desemba 26

# JUU KULIKO MIMI

**Wafilipi2:3**
**Msitende neno lolote kwa kushindana wala kwa majivuno; bali kwa unyenyekevu, kila mtu na amhesabu mwenziwe kuwa bora kuliko nafsi yake.**

Vipi kama umefika kazini au chuo kikuu na kukuta mwigizaji bora zaidi duniani kama msimamizi au mhadhiri wako aliyesimama? Wengi wangechukua hatua ya ziada kuwafanya wajisikie wamekaribishwa, wengine wanaweza hata kuacha chakula chao cha mchana ili tu kuwaheshimu. Mstari wa leo unakuambia fanya hivyo kwa KILA MTU!

Neno “amhesabu” linatokana na neno la Kigiriki hēgéomai , likimaanisha kuhesabu au kuzingatia. Inamaanisha kushikilia kwa makusudi mtazamo wa juu juu ya wengine, kuunda jinsi unavyowatendea, maarufu au la. Hebu wazia kama sisi sote tungeishi kwa njia hii, tukijinyenyekeza kuwaona wengine kuwa juu yetu wenyewe, matatizo mengi ya ulimwengu yangetoweka.

Tunapoanza kuangazia mwaka mpya, jitolee kuheshimu wengine kuliko wewe mwenyewe na kutanguliza mahitaji yao. Sio tu itashughulika na ubinafsi ndani yako, lakini pia itawafundisha wale walio karibu nawe somo kuu la kujitoa kwa ajili ya wengine!

**TAMKO LA KINABII**
Katika mwaka huu unaokuja, nitaonyesha kutokuwa na ubinafsi kuliko hapo awali. Watu watamwona Kristo kupitia kwangu katika Jina la Yesu! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
James 4:6

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: 1 Jn 3:13-5:21; 2 Jn , 3 Jn; Jude 1:1-16



Jumamosi, Desemba 27

# SALAMA KATI YA MBWA MWITU

**Luka 10:3**
**Enendeni, angalieni, nawatuma kama wana-kondoo kati ya mbwa-mwitu.**

Kutumwa kama mwana-kondoo kati ya mbwa mwitu kunaweza kusiwe na faida kubwa. Maana hata hivyo, mbwa mwitu hula wana-kondoo. Unaona, kondoo huwa katika hatari, lakini tu kama vile mchungaji anayewachunga.

Bwana Yesu Kristo, Mchungaji wetu Mwema, alitoa maisha yake ili tuwe na uzima tele (Yohana 10:10-11). Anautoa uhai Wake ili kuulinda uhai wako, akikulinda kutokana na hatari ya mbwa-mwitu wakali. Alilipa bei ghali zaidi kulinda na kuhifadhi maisha yako kutokana na madhara.

Uko chini ya ulinzi na mwongozo wa Mchungaji Mwema. Yeye hakupeleki peke yako na hatakuacha kamwe, kwa hivyo usiogope hatari. Unapotazamia mwaka mpya, Mchungaji wako Mwema yuko nyuma yako!

**TAMKO LA KINABII**
Ninapoiongoza siku yangu, hakuna hatari inayoweza kunigusa mimi na familia yangu. Ninaongozwa na Mchungaji wangu Mwema, ambaye tayari amenilinda na kuniepusha na hatari. Haleluya! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Ezekiel 34:11-16

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Yuda 1:17-25; Ufunuo 1-4



Jumapili, Desemba 28

# MGAO WA KIUNGU

**Deuteronomy 29:5**
**Nami miaka arobaini nimewaongoza jangwani; nguo zenu hazikuchakaa juu yenu, wala kiatu chako hakikuchakaa katika mguu wako.**

Watu wa Mungu waliposafiri kwenda nchi ya ahadi, nguo zao hazikuchakaa, na viatu vyao havikuchakaa. Huo ni mgao wa Ki-Ugu! Usipuuze ukweli kwamba ilidumu miaka arobaini, siku 14,600 za ugavi wa ajabu!

Katika hali ya kawaida, viatu vinapaswa kubadilishwa kila baada ya miezi nane hadi kumi na mbili. Lakini viatu vya wana wa Israeli vilidumu miezi 480 bila kuhitaji kubadilishwa! Je, walibaki na umri uleule au walibaki na ukubwa sawa wa mguu katika miaka hiyo arobaini? Hapana. Miili bado ilikua, ikasitawi, na kubadilika, lakini Mungu aliitegemeza kwa njia isiyo ya kawaida, hawakuwahi kuwa na wasiwasi juu ya mahitaji yao. Hiyo ilikuwa mgao wa Agano la Kale. Si zaidi Mungu atayokufanyia wewe uliyezaliwa mara ya pili? Usiwe na wasiwasi, Mungu ni mpaji daima, bila kujali hitaji!

**TAMKO LA KINABII**
Ninatabiri upaji usio wa kawaida kuwa kawaida katika maisha yangu! Sitakosa kitu chochote kizuri mnamo 2026! Ghala yangu itakuwa imejaa kila wakati, na nguo zangu zitafurika! Familia yangu imebarikiwa katika Jina la Yesu! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
2 Wakorintho 9:8

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Ufunuo 5:1-9:11



Jumatatu, Desemba 29

# DHAMANA YA MUNGU

**Waefeso 1:13**
**Nanyi pia katika huyo mmekwisha kulisikia neno la kweli, habari njema za wokovu wenu; tena mmekwisha kumuamini, yeye, na kutiwa muhuri na Roho yule wa ahadi aliye Mtakatifu.**

Katika mauzo ya kampuni, watengenezaji wanaoaminika hutangaza bidhaa zao kwa majina yao na mara nyingi hutoa dhamana, wakionyesha imani katika ubora wao kwa kuahidi kuzirekebisha au kuzibadilisha ikiwa zitaharibika ndani ya muda fulani.

Vivyo hivyo, umetiwa alama na kutiwa muhuri na mtengenezaji wa ulimwengu! Kazi ya Mungu ndani yako haina dosari, na dhamana Yake juu ya maisha yako haina ukomo. Shambulio lolote la adui anayejaribu kuvunja, kuharibu, au kukatisha maisha yako kamwe halitafanikiwa. Maisha yako yamefunikwa kikamilifu na dhamana ya Ki-Ungu ya Mungu, kuhakikisha matatizo hayaingii kwenye lango lako. Unapotembea katika uhalisi huu wa kiroho wa yule Aliyekufanya, utastawi zaidi ya fikra zako za ajabu!

**TAMKO LA KINABII**
Mimi ni zao la uwezo wa Mungu wa kuumba! Mungu, muundaji mkuu, ameweka kizuizi cha milele kwa adui ili kwamba yeyote akijaribu kunigusa, asinidhuru kwa Jina kuu la Yesu! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Isaya 54:17

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Ufunuo 9:12-14:8



Jumanne, Desemba 30

# UMECHAGULIWA

**Judges 6:15**
**Akamwambia, Ee Bwana, nitaokoa Israeli kwa jinsi gani? Tazama, jamaa zangu ndio walio masikini sana katika Manase, na mimi ndimi niliye mdogo katika nyumba ya Baba yangu.**

Maandiko ya leo, kuhusu Gideoni, yanafunua ukweli muhimu wa kiroho wenye umuhimu katika kutembea kwako kwenye mafanikio na Kristo. Wakristo wengi wanajiwekea mipaka kwa viwango vilivyowekwa na wengine, mazingira yao, au misimamo yao ya kijamii. Wanatilia shaka wito wa Mungu kwa sababu wamekubali maoni ya ulimwengu kuhusu wao ni nani. Lakini vikwazo unavyovifikiri ndio njia bora kwako kuwa mlinzi wa familia yako.

Hebu wazia kama Gideoni angeendelea kushikamana na maoni ya wengine kumhusu, ushindi mwingi sana ungepotea, yote hayo kwa sababu alidharau thamani yake kwa Mungu! Tunapofunga mwaka, tambua kwamba chaguo la Mungu kwako linatosha kuvunja kila kizuizi katika mwaka mpya. Alikuchagua kama mmoja wao, na atakutumia sana kwa kazi ya Ufalme iliyo mbele yake!

**TAMKO LA KINABII**
Umri wangu haujalishi; utamaduni wangu, asili yangu, jinsia, au rangi haileti tofauti inapofikia kiwango cha baraka nitakazopata katika mwaka mpya! NIMECHAGULIWA! Haleluya. Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Yoshua 1:9

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Ufunuo 14:9-18:24



Jumatano, Desemba 31

# ANZA KUANDIKA

**Zaburi 45:1**
**...Ulimi wangu ni kalamu ya mwandishi mstadi.**

Ukijaribu kutuma hundi tupu kwa benki, mtu wa benki atasema ni batili, haina chochote kilichoandikwa. Kwa hiyo unafanya nini? Unaijaza. Mungu amekupa hundi tupu, leo siku ya mwisho wa mwaka, uko huru kuijaza na kile unachotamani kwa mwaka mpya. Sulemani alipopokea hundi yake tupu, alisema haja yake, na mara moja, Mungu akamwambia imekubaliwa!

Kwa sasa, kwa ulimi wa mwandishi aliye tayari, jaza hundi na kurasa tupu za 2026. Tumia kalamu ya ulimi wako kuanza kuzungumza hadi mwaka mpya, ukichora ramani kila zamu utakayofanya. Weka alama kwa kila hatua muhimu na muda unaotaka. Tamka ustawi, afya ya Ki-Mungu, furaha na kila jambo jema. Unachosema ndivyo mwaka utakavyokuwa!

Ulete 2026!

**TAMKO LA KINABII**
Mwaka huu mpya utakuwa mwaka wangu wa kubainika. Ninatangaza maisha yangu kuwa mazuri! Sitalia machozi ya huzuni, wala sitakosa usingizi hata siku moja. Mwaka wangu umepangwa kwa Jina la Yesu! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Mithali 18:21

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA KWA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Ufunuo 19-22

NNA NABII
UEBERT ANGEL

# BWANA WETU YESU KRISTO

Bwana wetu Yesu Kristo ndiye msingi wa imani ya Kikristo, maisha yake na mafundisho yake yameathiri sana mwenendo wa historia. Bwana wetu Yesu Kristo anajulikana kwa huruma yake isiyo na kifani, hekima, na matendo ya miujiza Aliyofanya. Ujumbe wake ulijikita katika upendo, msamaha, na ahadi ya uzima wa milele, ukitoa tumaini na ukombozi kwa wote wanaomwamini. Katika huduma Yake yote, Alisafiri katika nchi za Yudea, akiwaponya wagonjwa, akiwafariji walioteseka, na kufundisha kuhusu ufalme wa milele wa Mungu.

Kumpokea Yesu Kristo kama Bwana na Mwokozi wako binafsi kunamaanisha kukubali mafundisho Yake na kualika uwepo Wake wa mabadiliko maishani mwako. Ni safari ya kuelekea utimilifu wa kiroho, yenye msingi katika imani, upendo, na ahadi ya wokovu.

Kupitia Bwana wetu Yesu Kristo, tunapata nguvu, tumaini, na njia ya amani ya milele. Kufanywa mkamilifu, au kuokolewa, ni kujisalimisha kwa Mungu na mpango na kusudi lake kwa maisha yetu. Ni kugeuka kutoka kwenye njia zetu za zamani na kumgeukia Yesu Kristo, kumwomba msamaha kutoka kwenye dhambi zetu na kuomba atupe maisha mapya ndani yake.

Warumi 10:9 inasema:
"Ukikiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka."

Wokovu ni zawadi ya bure ya Mungu kwetu na tunakuwa watoto wake. Ni kibali kisichoweza kubatilishwa cha kuwa familia ya Mungu na ni uwezeshwaji wa kuishi maisha kwa ujumla na kikamilifu kwa kusudi la kumwakisi Mungu kwa uumbaji Wake wote.

# JE, TAYARI UMEMPOKEA YESU KRISTO?

TUNAKUALIKA KUMFANYA YESU KRISTO KUWA BWANA WA MAISHA YAKO KWA KUOMBA OMBI HII;

"Ee BWANA MUNGU, NINAKUJA KWAKO KATIKA JINA LA YESU KRISTO. NINAAMINI KWA MOYO WANGU WOTE KATIKA YESU KRISTO MWANA WA MUNGU ALIYE HAI. NAAMINI ALI-KUFA KWA AJILI YANGU NA MUNGU AKAMFU-FUA KUTOKA KWA WAFU. NAAMINI YUPO HAI LEO. NINAKIRI KWA KINYWA CHANGU KWAMBA YESU KRISTO NDIYE BWANA WA MAISHA YANGU TANGU LEO.KATIKA YEYE NA KWA JINA LAKE NINA UZIMA WA MILELE, NI-MEZALIWA UPYA. ASANTE BWANA KWA KUIO-KOA NAFSI YANGU. MIMI SASA NI MTOTO WA MUNGU. HALELUYA!"

HONGERA SANA!
SASA WEWE NI MTOTO WA MUNGU.

To receive more information on how you can grow as a Christian, please get in touch with us on

**UK: +44 3333 448 612 / USA +1 240 781 6942**
**RSA +27 51 004 0209**

www.uebertangel.org | www.goodnewsworld.com

# AYA YA MAANDIKO KWA AJILI YA ULINZI

## ISAYA 54:

**14** NIMEJENGWA IMARA, NIKATHIBITIKA KATIKA HAKI. MBALI NA SHIDA YOYOTE--HAKUNA CHA KUOGOPA! MBALI NA HOFU-_HATA HAITANIKARIBIA!

**15** MTU YEYOTE AKINISHAMBULIA, HATA SITAFIKIRI KWAMBA MUNGU AMEMTUMA. NA IKIWA YEYOTE ATANISHAMBULIA, HAKUNA LITALOTOKEA.

**16** MUNGU ALIMUUMBA MUHUNZI AFUKUTAYE MOTO WA MAKAA NA KUFUA SILAHA ILIYOUNDWA ILI KUUA. PIA ALIMUUMBA MUHARIBU.

**17** LAKINI HAKUNA SILAHA INAYOWEZA KUNIDHURU AMBAYO IMEWAHI KUUNDWA. YEYOTE ATAKAYENITUHUMU ATAONDOLEWA KUWA NI MUONGO. MIMI NI MTUMISHI WA MUNGU HIVYO NDIYO NINAYOWEZA KUTARAJIA MUNGU KWAMBA ATAONA ILI KUHAKIKISHA KILA KITU KINAFANYA KAZI KWA AJILI YA MEMA YANGU.

**HIKI NDICHO MUNGU ANASEMA KWANGU NA HAKITASHINDWA KWA JINA LA YESU!**

TRANSLATED FROM THE MESSAGE BIBLE IN ENGLISH

# MWONGOZO WAKO WA KINABII WA KILA SIKU

Gazeti la GoodNews Daily sasa linapatikana katika matoleo kwa ajili ya vijana na watoto, pamoja na toleo kuu, likitoa neno lako la kinabii la kila siku moja kwa moja kutoka moyoni mwa Nabii Uebert Angel. Ibada hizi zimekusudiwa kuleta Neno la Mungu kwa uzima kwa kila mtu katika familia yako. Toleo la watoto linatanguliza imani, upendo na ahadi za Mungu kwa njia ya kufurahisha na ya kuvutia, huku toleo la vijana likitoa maarifa ya kina ili kuwaongoza maishani kwa hekima na nguvu za kiroho. Kila siku, pokea mwongozo wa kinabii unaolingana na matembezi yako na Mungu, haijalishi una umri gani! Usikose fursa hii na upate nakala yako bure leo.




SCAN ME

**IMEANDIKWA NA NABII UEBERT ANGEL**

@GOODNEWSDAILYDEVOTIONAL

WWW.GOODNEWSDAILYDEVOTIONAL.COM

# MUUNGANISHO WA HABARI NJEMA

NUNUA NAKALA YAKO LEO!




Ufuatiliaji wa Neno la Mungu: kufungua utajiri wa kiroho kupitia muunganisho wa habari njema. Katika kutafuta maisha yenye mizizi ndani ya Kristo,
Kusimama bila kuyumba-yumba kwenye Neno la Mungu huwa jiwe kuu la msingi. Jarida la muunganisho wa habari njema, toleo la kwanza linatoa nyenzo isiyo na kifani kwa safari hii, ikipanga injili kwa ustadi katika sehemu za mada kwa masomo yaliyoboreshwa na kuelewa kwa urahisi.

Imeandikwa na Nabii Uebert Angel

WWW.GOODNEWSDAILYDEVOTIONAL.COM

# KARIBU KWENYE KITOVU CHETU CHA MTANDAONI!
# NA NABII UEBERT ANGEL

TEMBELEA TOVUTI YETU

WWW.GOODNEWSDAILYDEVOTIONAL.COM

@GOODNEWSDAILYDEVOTIONAL




Pata uongozi wa kila siku na ukuaji wa kiroho kwa kutembelea tovuti ya Habari Njema Kila Siku. Ingia katika Neno lako la kinabii la siku na maudhui yenye kutajirisha ambayo yanaweza kubadilisha maisha yako. Usikose nafasi ya kuimarisha imani yako na kupata furaha ndani ya Neno la Mungu. Tembelea tovuti ya habari njema leo!

For more information visit: www.goodnewsdailydevotional.com
You can also send an email to: gnd@goodnewsworld.com
Or Call At: **USA: +1 (240) 781-6942 UK: +44 333 344 8612**
**ZW: +263 773 195 955 RSA: +27 (51) 004-0209**




# KILA SIKU

Spotify

Jiunge na jumuiya yetu ya wasikilizaji wa kimataifa ambao huanza siku kwa habari njema kilasiku. Sikiliza Habari Njema kwenye Spotify na uambatane nayo kwenye ukuaji wa kiroho na ukweli wa kibiblia chini ya ufunuo na mafundisho ya Nabii Uebert Angel.




# KILA SIKU

Youtube

Tunakuletea shuhuda za maisha halisi kuhusu matokeo ya Habari Njema Kila Siku ibada imekuwa duniani kote kupitia chaneli yetu ya YouTube. Kama shajala nambari moja ya kila siku, imegusa maisha ya kutosha, ikieneza ujumbe wa tumaini, upendo na imani. Kupitia mafundisho mazito ya nabii Uebert Angel, shajala ya habari njema kila siku imekuwa chombo chenye nguvu cha kibinafsi cha mageuzi, kuhamasisha watu binafsi, familia, na watoto kuishi maisha yao kusudi na utimilifu.

**Imeandikwa na Nabii Uebert Angel**

SUBCRIBE NOW

@GOODNEWSDAILYDEVOTIONAL

WWW.GOODNEWSDAILYDEVOTIONAL.COM




# DHAMINI LUGHA

Jiunge nasi katika safari hii ya ajabu kwa kufadhili na kushiriki Shajala la habari njema kila siku ili tuweze kupenya mioyo ya mamilioni kote ulimwengu. Kwa pamoja, tunaweza kueneza ujumbe wa habari njema ya neema ya Mungu kwa kila jiji, kila mtaa, na kaya katika lugha nyingi kote ulimwenguni. Kila mwezi, washirika wetu waliojitolea husambaza nakala za habari njema Kila Siku bila malipo kwa watu katika vituo vya watoto yatima, magereza, hospitali, nyumba za wazee, shule, taasisi za serikali, na maeneo mengine mengi duniani kote. Tumepokea shuhuda za wokovu, uponyaji, upokeaji wa kiungu, na mengine zaidi kutokana na kampeni hii ya kimataifa ya usambazaji. Kuwa sehemu ya hii hatua tukufu ya Mungu kwa kumpa mtu nafasi ya kuanza upya na matumaini ya kesho.

NA NABII UEBERT ANGEL

**@GOODNEWSDAILYDEVOTIONAL**

**SPONSOR AT: WWW.GOODNEWSDAILY DEVOTIONAL.COM**

**INAPATIKANA KATIKA LUGHA NYINGI**

# DIRA YA KIDUNIA INAHITAJI BAJETI YA ULIMWENGU

**KUWA MPENZI WA HABARI NJEMA KILA SIKU**



Kupitia ushirikiano wako wa ukarimu na usaidizi wa kifedha tunaweza kushiriki habari njema kila kona ya dunia na kuwaambia wasiosimuliwa kuhusu habari njema wa ufunuo wa Bwana wetu Yesu Kristo kama ulivyofundishwa na Nabii Mtukufu Uebert Angel. Tunaweza kutafsiri, kuchapisha, na kusambaza shajala la habari njema kila siku kupitia Safari zetu za Misheni, Kampeni ya habari njema On-The-Go, na kufadhili kampeni ya Taifa/Lugha ili kusaidia zaidi kueneza injili. Kuwa mshirika na mshikadau katika maono haya ya kimataifa na ujiunge nasi katika kupeleka ujumbe wa Mungu kwa mataifa kote ulimwenguni kupitia Mtume wetu Malaika, Habari Njema Kila Siku.

**Na Nabii Uebert Angel**

@GOODNEWSDAILYDEVOTIONAL

**PARTNER AT: WWW.GOODNEWSDAILYDEVOTIONAL.COM**



For further information on how to grow as a Christian, please get in touch with us at:

UK: +44 3333 448 612
USA +1 240 781 6942
RSA +27 51 004 0209
ZWE +263 773 195 955

**gnd@goodnewsworld.com**
**goodnewsdailydevotional.com**

**SCAN FOR YOUR FREE DOWNLOAD**